

**DUA
ZA
MWEZI WA RAMADHAN**

Kimekusanywa na:
Tayyiba Publishers – Canada

Kimetarjumiwa na:
Ustadh Haji Hemedi Lubumba Selemani
Na
Al-Haj Ramadhani S. K. Shemahimbo

© **Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
AL-ITRAH FOUNDATION

ISBN: 978 – 9987 – 17 – 035 – 7

Kimekusanywa na:
Tayyiba Publishers - Canada
Barua Pepe: tayyiba.publishers@gmail.com

Kimetarjumiwa na:
Ustadh Haji Hemedi Lubumba Selemani
Na
Al Hajj Ramadhani S. K. Shemahimbo

Toleo la Kwanza: June, 2016
Nakala: 1000

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640 / 2127555
Barua Pepe: alitrah@yahoo.com
Tovuti: www.alitrah.info

YALIYOMO

Neno la Mchapishaji	1
Dua katika Mwezi wa Ramadhani Tukufu.....	3
Dua Uonapo Mwezi Mwandamo Wa Ramadhani.....	5
Dua Za Usiku wa Ramadhani	8
Dua ya Kwanza.....	8
Dua ya Pili.....	12
Maelezo Mafupi Juu Ya Dua Ya Al-Iftitah:.....	15
Kumtukuza Mwenyezi Mungu:	16
Msisitizo Juu Ya Upweke (Tawhiid) Wa Allah:	16
Ukarimu Wa Mwenyezi Mungu:	16
Mahusiano Ya Allah Na Wanadamu:	17
Kumswalia Mtukufu Mtume (Salawat):	17
Rehma Na Amani Juu Ya Ma'sumiin:	18
Jukumu La Imam Wa Kumi Na Mbili (A.S.):	15
Dua Ya Tatu.....	20
Dua Ya Nne : Dua Al-Iftitah	22
Dua Ya Tano.....	55
Dua Ya Sita.....	60
Dua Ya Saba.....	63

Dua Ya Sahri (DAKU)	64
Ziyara Al-Waritha	68
Ziyara Ya Ali Akbar (A.S.).....	74
Ziyara Ya Wahanga Wote	75
Ziyara Ya Abul-Fadhli Abbas (A.S.).....	78
Dua Baada Ya Ziyara	80
Dua Za Kila Siku Ya Ramadhani	83
Mwezi Mosi:	83
Mwezi Pili:	84
Mwezi Tatu:	84
Mwezi Nne:	85
Mwezi Tano:	86
Mwezi Sita:	87
Mwezi Saba:	87
Mwezi Nane:	88
Mwezi Tisa:	89
Mwezi Kumi:	89
Mwezi Kumi Na Moja:	90
Mwezi Kumi Na Mbili:	91
Mwezi Kumi Na Tatu:	92
Mwezi Kumi Na Nne:	92

Mwezi Kumi Na Tano:	93
Mwezi Kumi Na Sita:	94
Mwezi Kumi Na Saba:	94
Mwezi Kumi Na Nane:	95
Mwezi Kumi Na Tisa:	96
Mwezi Ishirini:	96
Mwezi Ishirini Na Moja:	97
Mwezi Ishirini Na Mbili:	98
Mwezi Ishirini Na Tatu:	99
Mwezi Ishirini Na Nne:	99
Mwezi Ishirini Na Tano:	100
Mwezi Ishirini Na Sita:	101
Mwezi Ishirini Na Saba:	101
Mwezi Ishirini Na Nane:	102
Mwezi Ishirini Na Tisa:	103
Mwezi Thelathini:	104
Dua Ya Mikesha Kumi Ya Mwisho.....	105
Kithirisha Maneno Haya:	111
Dua Ya Usiku Wa Mwezi Ishirini Na Moja	112
Dua Ya Usiku Wa Mwezi Ishirini Na Mbili.....	116
Dua Ya Usiku Wa Mwezi Ishirini Na Tatu.....	121

DUA ZA MWEZI WA RAMADHAN

Dua Ya Usiku Wa Mwezi Ishirini Na Nne	125
Dua Ya Usiku Wa Mwezi Ishirini Na Tano	130
Dua Ya Usiku Wa Mwezi Ishirini Na Sita	134
Dua Ya Usiku Wa Mwezi Ishirini Na Saba	138
Dua Ya Usiku Wa Mwezi Ishirini Na Nane	143
Dua Ya Usiku Wa Mwezi Ishirini Na Tisa	147
Dua Ya Usiku Wa Mwezi Thelathini.....	151

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kdua (Kiarabu/Kingereza) kwa jina la A Manual of Ramadhan Devotion. Sisi tumekiita, Du'a za Mwezi wa Ramadhani.

Kitabu hiki ni mkusanyiko wa dua maarufu zinazosomwa katika mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Jambo bora kabisa ambalo muumini anaweza kuomba wakati wa mwezi huu ni maghfira na msamaha kutokana na dhambi zake zilizopita. Nyingi ya dua maalumu kwa mwezi wa Ramadhani ni za kuomba msamaha wa mzigo mkubwa wa dhambi ambao mtu ameubeba.

Ramadhani ni nafasi nzuri sana aliyopewa yeye kufanya madhambi yake yafutwe na kujipatia cheo cha juu mbele ya macho ya Mwenyezi Mungu.

Kutokana na umuhimu wa dua hizi, tumeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili, kwa lengo letu lile lile la kuwahudumia ndugu zetu Waislamu wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu Ustadh Al Haji Hemedi Lubumba Selemani na Al Haji Ramadhani S. K. Shemahimbo, kwa kukubali jukumu hili la kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki katika kusahihisha na kukipitia hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa ni chenye manufaa kwa wasomaji wetu na kuzidisha upeo wao wa ibada na elimu katika dini.

SHUKRANI MAALUMU

Wachapishaji wa kwanza wa kitabu hiki katika lugha ya Kiarabu /
Kiingereza ni:

**Tayyiba Publishers
Canada**

Barua pepe: tayyiba.publishers@gmail.com

Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation inaishukuru sana Taasisi hii
kwa kutukubalia tukitarjumi kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili.
Tunamuomba Allah ‘Azza wa Jalla awazidishie kila la kheri wazidi
kuendeleza kazi hii ya tablighi ulimwenguni kote -Amin.

Mchapishaji:

Alitrah Foundation.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

DUA KATIKA MWEZI WA RAMADHANI TUKUFU

Mwezi wa Ramadhani ni fursa iliyotolewa na Muumba Mwenye huruma kwa ajili ya waja wake kujikurubisha karibu Naye, kuomba msamaha kwa ajili ya dhambi zao, na ukidhiwaji wa haja zao. Ndani ya Qur’ani Tukufu, katikati ya mjadala muhimu juu ya mwezi wa Ramadhani, Aya ifuatayo, ambayo ni dhahiri kwamba haina uhusiano wa moja kwa moja na Ramadhani, imeingizwa: **“Na waja wangu watakapokuuliza juu yangu basi hakika mimi nipo karibu, nayaitika maombi ya muombaji anaponiomba, basi waniitikie na waniamini, ili wapate kuongoka. (2:186)**

Wafasiri wanakubaliana kwamba hii ni Aya yenye nguvu sana kati ya Aya zote juu ya uhusiano wa ki-ungu na binadamu. Aya yote imesimama katika kiwakilishi nomino cha umoja (singular) nafsi ya kwanza, ambayo imerudiwa mara saba. Ni uthibitisho wa ule uhusiano wa karibu sana baina ya mwanadamu na Muumba wake, na uhakikisho kwamba yeye atasikilizwa pale atakapokuwa anamuomba Yeye (s.w.t).

Kwamba Aya kama hii ni lazima ijumuishwa miongoni mwa Aya zinazozungumzia umuhimu wa mwezi wa Ramadhani, na baadhi ya kanuni zake (tazama 2:182-7), ni dalili ya dhima muhimu ya Dua katika mwezi wa Ramadhani. Kujizulia kutokana na kukidhi mata-manio ya kimwili kunachochea kuongezeka kwa imani ya kiroho, na kunasababisha mwelekeo juu Swala na ibada kwa jumla.

Waumini hujihisi kuwa karibu na Mwenyezi Mungu, na Mungu huwakumbusha kwamba na Yeye pia yuko karibu, na atayajibu maombi na Dua zao. Masiku (mikesha) ya mwezi wa Ramadhani hutumika kwa kukesha katika swala na Dua kwa wingi. Hata wale waumini ambao kwa kawaida hawana muda mwingi kwa ajili ya Dua, wanajaribu kufanya hivyo katika mwezi huu. Hii ni kwa sababu ya msisitizo wa utukufu wa mwezi huu, na ile ahadi ya thawabu za ziada, na vilevile ule uhakikishiwaji wa majibu mazuri ya mafanikio. Anasema Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “.....fanya maombi ukiwa umenyanyua mikono yako juu kwani hizi ndio nyakati bora zaidi, ambazo kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anawaangalia waja wake kwa huruma, anajibu Dua zao kama wakiomba, anaitika kama wanamwita, anatoa kama wakiomba na anawakubalia kama wakimsihi (hadithi ya Mtume anapoukaribisha mwezi wa Ramadhani).

Jambo bora kabisa ambalo muumini anaweza kuomba wakati wa mwezi huu ni maghfira, msamaha juu ya dhambi zake zilizopita. Nyingi ya Dua maalum kwa mwezi wa Ramadhani ni za kuomba msamaha wa mzigo mkubwa wa dhambi ambao mtu ameubeba. Ramadhani ni nafasi nzuri sana aliyopewa yeye kufanya madhambi yake yafutwe, na kujipatia cheo cha juu mbele ya macho ya Mwenyezi Mungu. Hivyo watu wengi wanasamehewa katika mwezi huu kiasi kwamba ni wale wasio na bahati tu ambao wanakoseshwa. Mtukufu Mtume anasema katika hadithi hiyo hiyo: “Hakika mwenye majuto ni yule ambaye anakosa msamaha wa Mwenyezi Mungu katika mwezi huu mashuhuri.” Mambo mengine ya kuomba ni pamoja na kukidhiwa haja, kuondolewa mateso, na mafanikio katika akhera.

DUA UONAPO MWEZI MWANDAMO WA RAMADHANI

Mwenyezi Mungu ameagiza kwamba Waislamu watumie mwendo wa mwezi ili kutambua upitaji wa miezi na miaka. Wakati wale Waislamu wa mwanzo walipoulizwa juu ya mwezi mpya (mwandamo), Mwenyezi Mungu akashusha Aya isemayo: Mwenyezi Mungu asema:

يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْأَهْلِ قُلْ هِيَ مَوَاقِيتُ لِلنَّاسِ
وَالْحَجِّ {189}

“Wanakuuliza juu ya miezi: Sema : Hivyo ni (vipimo asilia) vya nyakati kwa ajili ya (mfumo wa maisha ya) watu na Hijja .(2:189)

Mwezi mwandamo wa Ramadhani ni makhsusi kwa Waislamu.

Unatangaza kuanza kwa mwezi mtukufu huo na kuanza kwa rehema na neema zinazohusiana na Ramadhani. Kwa mujibu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) yeyote yule anayeona mwezi mwandamo wa Ramadhani anapaswa kusoma Dua ifuatayo.*

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema
Mwenye kurehemu.**

رَبِّي وَرَبُّكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ

**Mlezi wangu na Mlezi wako ni Allah, Mwenyezi
Mungu, Mola Mlezi wa viumbe.**

اللَّهُمَّ أَهْلُهُ عَلَيْنَا بِالْأَمْنِ وَالْإِيمَانِ

**Ewe Mungu wangu! Uandamishe kwetu kwa amani
na imani.**

وَالسَّلَامَةِ وَالْإِسْلَامِ

Kwa salama na unyenyekevu.

وَالْمُسَارَعَةِ إِلَى مَا تُحِبُّ وَتَرْضَى

**Na kwa kuharakisha kuyaendea yale uyapendayo na
kuyaridhia.**

اللَّهُمَّ بَارِكْ لَنَا فِي شَهْرِنَا هَذَا

**Ewe Mungu wangu! Tupe baraka ndani ya mwezi
wetu huu.**

وَأَرْزُقْنَا خَيْرَهُ وَعَوْنَهُ

Turuzuku kheri yake na msaada wake.

وَاصْرِفْ عَنَّا ضُرَّهُ وَشَرَّهُ وَبَلَاءَهُ وَفِتْنَتَهُ

**Na tuepushie madhara yake, shari yake, balaa lake na
mtihani wake.**

DUA ZA USIKU WA RAMADHANI

Kila usiku wa mwezi wa Ramadhani ni wakati wa kumwabudu Allah (s.w.t.). kwa kumuomba na kutaka msamaha Wake. Mwenyezi Mungu anajua kwamba wanadamu wana uwezekano wa kutenda dhambi, na wanahitaji fursa na wasaa wa kutubia na kujirekebisha.

Hivyo mwezi wa Ramadhani ni msimu wa Dua na kuomba maghufira ambapo Waislamu wanajivua mizigo ya dhambi. Dua zinazofuata zimefundishwa na Ma'sumiin (a.s.) na zinatunyeshwa sisi namna ya kutafuta msamaha na Huruma za Allah katika mwezi huu.

DUA YA KWANZA

Baada ya kumtukuza Mwenyezi Mungu, Dua inayofuata inaelezea ubora wa mwezi wa Ramadhani, na sifa zake bainifu. Wenye kuabudu na wenye kuomba wanapata upendeleo maalumu ikiwa wataomba ndani ya mwezi huu. Dua hii imependekwa pia baada ya Swala za wajibu.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.**

يَا عَلِيُّ يَا عَظِيمُ

Ewe Uliye juu! Ewe Mwenye uwezo!

يَا غَفُورُ يَا رَحِيمُ

Ewe Msamehevu! Ewe Mrehevu!

أَنْتَ الرَّبُّ الْعَظِيمُ

Wewe ni Mola Mlezi uliye na uwezo,

الَّذِي لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ

Ambaye hakuna yeyote mfano Wake,

وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

Na Yeye ni Msikivu, Mjuzi.

وَهَذَا شَهْرٌ عَظُمَتْهُ وَكَرَّمَتْهُ

Huu ni mwezi ulioutukuza na kuupa heshima,

وَشَرَّفَتْهُ وَفَضَّلَتْهُ عَلَى الشُّهُورِ

Ulioupa sharafu na ubora kuliko miezi mingine,

وَهُوَ الشَّهْرُ الَّذِي فَرَضْتَ صِيَامَهُ عَلَيَّ

Nao ni mwezi ambao umefaradhisha funga juu yangu,

وَهُوَ شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أَنْزَلْتَ فِيهِ الْقُرْآنَ

**Nao ni mwezi wa Ramadhan ambao ndani yake
umeteremsha Qur'an,**

هُدًى لِلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِّنَ الْهُدَى وَالْفُرْقَانِ

**Ili kuwa mwongozo kwa watu, na dalili zilizo wazi za
mwongozo na upambanuzi.**

وَجَعَلْتَ فِيهِ لَيْلَةَ الْقَدْرِ

Ndani yake umeweka Laylatul-Qadri,

وَجَعَلْتَهَا خَيْرًا مِنْ أَلْفِ شَهْرٍ

Na ukaufanya kuwa bora kuliko miezi elfu.

فِيَا ذَا الْمَنِّ وَلَا يُمَنَّ عَلَيْكَ

**Ewe Mwenye fadhila na wala hakuna yeyote mwenye
kukufadhili,**

مُنَّ عَلَيَّ بِفَكَكَ رِقَبَتِي مِنَ النَّارِ فِيمَنْ تَمُنُّ عَلَيْهِ

**Nifanyie fadhila kwa kuniepusha na moto. Niwe
miongoni mwa wale uwafanyiao fadhila,**

وَأَدْخِلْنِي الْجَنَّةَ بِرَحْمَتِكَ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ

**Na niingize Peponi kwa rehema zako ewe Mbora wa
wenye kurehemu.**

DUA YA PILI

(Kwa ajili ya kila usiku wa Ramadhani na kwa nyakati zote):

Moja ya taratibu za Dua ni kuwaombea wengine, kuwakumbuka wale ambao wana shida.

Ni kitendo kisicho na ubinafsi, kuonyesha ubinadamu na kuwafikiria wengine. Mwenyezi Mungu anampenda sana yule mtu anayewaombea wengine kwanza, halafu ndipo ajiombe yeye mwenyewe. Imam wa sita (a.s.) anasema: “Wakati Mwislamu anapomuombea ndugu yake, (nyongeza katika) riziki inatolewa kwake kwa wingi, mateso husukumiliwa mbali na yeye, na malaika wanamwambia: “Utapata nawe pia kama hayo hayo.”

Watu wengi duniani kote wanapatwa na matatizo yasiyoelezeka. Dhulma na uonevu vimeenea katika nchi nyingi. Ni kidogo sana tunachoweza kufanya ili kuyaondoa mateso hayo.

Hata hivyo, tunaweza angalau kuwaombea kwa kweli ya dhati, tukitegemea kwamba Mwenyezi Mungu atawasaidia kwani anao uwezo juu ya kila kitu. Na sisi vilevile tunamuomba Allah (s.w.t.), atatupatie nia na uwezo wa kuwasaidia wengine kwa njia yoyote tutakayoweza.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.**

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ

Ewe Mungu wangu! Mpe rehema Muhammad na Aali Muhammad.

اللَّهُمَّ ادْخِلْ عَلَى أَهْلِ الْقُبُورِ السُّرُورَ

Ewe Mungu wangu! Wape furaha watu wa makaburini.

اللَّهُمَّ اغْنِ كُلَّ فَقِيرٍ

Ewe Mungu wangu! Mtajirishe kila fakiri.

اللَّهُمَّ اشْبِعْ كُلَّ جَائِعٍ

Ewe Mungu wangu! Mshibishe kila mwenye njaa.

اللَّهُمَّ اكْسُ كُلَّ عُرْيَانٍ

Ewe Mungu wangu! Mvishe kila aliye tupu.

اللَّهُمَّ اقْضِ دَيْنَ كُلِّ مَدِينٍ

Ewe Mungu wangu! Mlipie deni kila mwenye deni.

اللَّهُمَّ فَرِّجْ عَن كُلِّ مَكْرُوبٍ

Ewe Mungu wangu! Mfariji kila mwenye matatizo.

اللَّهُمَّ رُدِّ كُلَّ غَرِيبٍ

Ewe Mungu wangu! Mrejeshe nyumbani kila mgeni.

اللَّهُمَّ فَكِّ كُلَّ آسِيرٍ

Ewe Mungu wangu! Mwachie huru kila mateka.

اللَّهُمَّ أَصْلِحْ كُلَّ فَاسِدٍ مِنْ أُمُورِ الْمُسْلِمِينَ

Ewe Mungu wangu! Sahihisha kila lisilo sawa miongoni mwa mambo ya Waisilamu.

اللَّهُمَّ أَشْفِ كُلَّ مَرِيضٍ

Ewe Mungu wangu! Mponye kila mgonjwa.

اللَّهُمَّ سُدِّ فَقْرَنَا بِغِنَاكَ

Ewe Mungu wangu! Ziba ufakiri wetu kwa utajiri Wako.

اللَّهُمَّ غَيِّرْ سُوءَ حَالِنَا بِحُسْنِ حَالِكَ

Ewe Mungu wangu! Badili ubaya wa hali yetu kwa uzuri wa hali Yako.

اللَّهُمَّ اقْضِ عَنَّا الدَّيْنَ وَاغْنِنَا مِنَ الْفَقْرِ

Ewe Mungu wangu! Tulipie deni na tusaide dhidi ya ufakiri.

إِنَّكَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

Hakika Wewe ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

MAELEZO MAFUPI JUU YA DUA YA AL-IFTITAH:

Dua al-Ifitah ilifundishwa na Imam wetu wa kumi na mbili (a.s.) kwa ajili ya Mashia kusoma kila usiku wakati wa mwezi wa Ramadhani. Dua hii ni bora sana kwa ajili ya kujenga mwelekeo wa mwanadamu kwa Mola Wake kwa vile inazungumzia vipengele vingi vya udhaifu wa binadamu, na neema za Allah. Dua hii inaweza kugawanyika katika sehemu mbili:

1. Uhusiano wa binadamu na Mwenyezi Mungu.
2. Viongozi wa ki-Ungu watakatifu.

Sehemu ya kwanza ya Dua hii inaelezea sifa mbalimbali za Mwenyezi Mungu, na inadhihirisha hali ya huruma na upendo wa Mwenyezi Mungu juu ya wanadamu. Sehemu hii ya Dua inaweza kugawanywa zaidi katika vifungu vifuatavyo:

KUMTUKUZA MWENYEZI MUNGU:

Kama ilivyo taratibu ya Dua, Dua hii ya al-Ifitah inaanza na kumsifu na kumtukuza Mwenyezi Mungu. Hii sio kwa sababu kwamba Mwenyezi Mungu anahitajia kusifiwa kabla ya Yeye kujibu Dua zetu, bali ni kumkumbusha muombaji juu ya yule Muweza wa yote anayeongea naye, na hatimaye kuweka hofu juu ya Allah katika nyoyo ambazo mara nyingi zinakuwa hazizingatii.

Uanzaji wa Dua hii unamuweka muombaji katikati ya matumaini na hofu, mtazamo bora wakati unapoomba. Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa huruma, lakini pia ni mkali wa kuadhibu. Binadamu wasiwe wenye kukata tamaa, wala wasijiamini sana bali wadumu katika Njia Yake.

MSISITIZO JUU YA UPWEKE (TAWHIID) WA ALLAH:

Mwenyezi Mungu hana mshirika wala mtoto, na anayo mamlaka kamili na udhibiti usiogawanyika, juu ya viumbe. Wakazi wa angani na mbinguni wanamtegemea Yeye. Hii ni kuimarisha utegemeaji wa muombaji juu ya Mwenyezi Mungu, kwani hakuna mwingine tena anayeweza kumgeukia.

UKARIMU WA MWENYEZI MUNGU:

Hazina za Mwenyezi Mungu hazifilisiki wala haziishi, na wakati wote zinatolewa kwa ukarimu juu ya viumbe Wake. Shida za binadamu ni nyingi mno, na kwa kuuwacha wazi mlango wa Du'a, Mwenyezi Mungu amewapa ufunguo wa kwenye hazina Zake. Milango Yake wakati wote iko wazi, na hakuna maombi yoyote Kwake yanayokataliwa bila ya majibu fulani.

Lakini mara nyingi mwanadamu ni mtovu wa shukurani, na wakati wote ni mlafi. Anategemea kwamba Du'a zake siku zote zitajibiwa mara moja. Wakati kuridhika kama huko hakupatikani, yeye anageuka, badala ya kujikumbusha yeye mwenyewe juu ya neema zote anazozifaidi.

MAHUSIANO YA ALLAH NA WANADAMU:

Ni uhusiano wa ajabu kweli kweli! Ingawa ni mwanadamu anayemhitaji Allah, na anapaswa kujitahidi kumuelekea Yeye; ni Mwenyezi Mungu anayemualika na kumhimiza yeye kuja, ambaye anaonyesha upendo na huruma na anaendelea kumpendelea kwa njia nyingi.

Kama anavyosema Imam wa nne katika Dua ya Abu Hamza Thumali: “Shukurani zimwendee Allah ambaye huniitikia mimi pale ninapomwita, ingawa mimi ninasitasita pale anaponiita, na sifa ni kwa juu Yake Allah ambaye hunipa mimi wakati ninapomuomba, ingawa mimi ni bakhili pale anaponiomba.” Hii inafaa kuitafakari kwa wale wanaomdhanja Mwenyezi Mungu kwamba ni bwana wa kidhalimu anayeweka sheria juu ya wanaadamu.

Sehemu hii ya Dua ni somo bora sana katika mtazamo wa Kiislami wa sifa za Mwenyezi Mungu. Mola wa Uislami ni mwenye upendo, Mungu mwenye huruma anayewatendea wanadamu kwa ubora zaidi kuliko wanavyostahili. Msingi wa uhusiano kati ya Mwenyezi Mungu na mwanadamu ni upendo wa Muumba juu ya viumbe Wake. Ni juu ya mwanadamu kuupekua moyo wake kwa ajili ya mwitiko wa kutendeanza. Sehemu ya pili ya Du'a hii inamtakia rehema na amani Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Ma'asumin wote, na halafu inazungumzia jukumu la Imam wa kumi na mbili (a.s.).

KUMSWALIA MTUKUFU MTUME (SALAWAT):

Baada ya imani juu ya Mwenyezi Mungu, sehemu muhimu ya dini inayofuata ni imani juu ya wale aliowatuma. Hivyo baada ya kukiri Ukuu na Upole wa Muumba, Du'a hii inatufundisha sisi kuwakiri wale viongozi wa Ki-Ungu watukufu kama viongozi wetu kuelekea kwa Allah (s.w.t.) Rehma na amani zinatamwa kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kama ishara ya mapenzi na shukurani kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kutambua kwamba yeye ni binadamu na anahitaji huruma na neema kutoka kwa Allah. Inaimarisha vilevile ukumbusho kwa Mtume (s.a.w.w.) na msukumo wa kuifuata njia yake.

REHMA NA AMANI JUU YA MA'SUMIIN:

Baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) warithi waandamizi wake wanakumbukwa na kuombewa. Hawa ndio viongozi halisi wa umma wa Kiislam ambao waliteuliwa na Mwenyezi Mungu. Imani juu yao, na upendo kwao ni sehemu muhimu ya imani ya ki-Shi'a.

JUKUMU LA IMAM WA KUMI NA MBILI (A.S.):

Katika kila zama Mwenyezi Mungu huwa anaye mwakilishi Wake ambaye anawaongoza viumbe Wake kwenye kusimamisha haki na uadilifu katika ardhi. Huyu Imam wa Kumi na mbili ndiye kiongozi wa zama zetu hizi, ambaye atakuja kudhihiri na dini ya Mwenyezi Mungu itashinda (dini zote) duniani.

Sehemu ya mwisho ya Dua al-Iftitah inazungumzia kuhusu kuja kwake, kuwaandaa waumini juu ya kusimama kwa utawala wa Allah unaotarajiwa juu ya ardhi. Kuomba msaada na ushindi kwa ajili ya Imam wa Kumi na mbili kunatukumbusha sisi kwamba tunamngojea yeye, na tunahitaji kujiandaa kwa ajili ya kuja kwake. Tunakuwa tunatambua wajibu wetu katika wakati wa kughibu (kufichika) kwake,

na umuhimu wa kujifundisha sisi wenyewe kama wasaidizi wake. Tunaomba kwa ajili ya ndoto ya mwisho ya Mwislam, hali ambayo dini ya Mwenyezi Mungu inapata umuhimu mkubwa, na ukafiri na unafiki vinadhalilishwa.

Dua al-Iftitah inatukumbusha sisi kwamba imani na vitendo vyote ni muhimu na vya lazima ili kuwa muumini halisi na wa kweli. Imani juu ya Mwenyezi Mungu inafungamana na kuufanyia kazi ujumbe Wake uliokuja na Mtume Wake, na kusimamisha dini Yake duniani. Wakati ambapo hilo linaweza kufanyika tu kupitia kwa Imam, sisi tunapaswa kufanya kazi na kuomba kwa ajili ya kudhihiri kwake. Wanadamu wanaweza kufaidi uadilifu na amani halisi, na kutimizwa kwa haja zao, chini ya kiongozi huyo Mtukufu.

Dua al-Iftitah sio maombi tu kwa ajili ya shida na haja zetu, bali ni ufundishaji wa mizizi ya imani, na upangaji kwa ajili ya namna ya maisha. Inabakia kwetu sisi kuandaa jedwali la maisha yetu wakati tunapoisoma du'a hii nzuri katika kila usiku wa Ramadhani.

DUA YA TATU

Dua Hii Kwa Kawaida Husomwa Kabla Ya Dua Al-Iftitah

Hii ni Du'a fupi lakini yenye manufaa makubwa sana. Ndani Yake tunamuomba kwamba Mwenyezi Mungu atujaalie fursa ya kwenda Hijja, na kwamba atusamehe dhambi zetu. Kuhiji kwenye nyumba ya Allah (s.w.t.) ni tendo kubwa sana la ibada na tamaa kuu ya kila Muislam. Imam Ali (a.s.) anasema kuhusu hujaji: “Yule anayekwenda Hijja na Umra ni mgeni wa Mwenyezi Mungu, na ni haki juu ya Mwenyezi Mungu kwamba amheshimu mgeni Wake, na anaonyesha mapenzi Yake kwake kupitia msamaha (wa dhambi).”

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.**

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ

**Ewe Mungu wangu! Mpe rehema Muhammad na Aali
za Muhammad.**

اللَّهُمَّ رَبَّ شَهْرِ رَمَضَانَ الَّذِي أَنْزَلْتَ فِيهِ الْقُرْآنَ

**Ewe Mungu wangu! Mola Mlezi wa mwezi wa
Ramadhan, ambao ndani yake uliteremsha Qur'an,**

وَأَفْتَرَضْتَ عَلَيَّ عِبَادِكَ فِيهِ الصِّيَامَ

Na humo ukafaradhisha funga kwa waja Wako.

صَلِّيْ عَلَيَّ مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ

Mpe rehema Muhammad na Aali za Muhammad.

وَارْزُقْنِي حَجَّ بَيْتِكَ الْحَرَامِ

Niruzuku kwenda kuhiji nyumba yako tukufu,

فِي عَامِي هَذَا وَفِي كُلِّ عَامٍ

Ndani ya mwaka huu na kila mwaka.

وَاعْفِرْ لِي تِلْكَ الذُّنُوبَ الْعِظَامَ

Nisamehe dhambi hizo kubwa.

فَإِنَّهُ لَا يَغْفِرُهَا غَيْرُكَ

**Kwa hakika hakuna yeyote asiye Wewe awezaye
kuzisamehe,**

يَا رَحْمَنُ يَا عَلَّامُ

Ewe Mwingi wa rehema Uliye Mjuzi mno.

DUA YA NNE : DUA AL-IFTITAH

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.**

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ

**Ewe Mungu wangu! Mpe rehema Muhammad na Aali
Muhammad.**

اللَّهُمَّ إِنِّي أفتَحُ الثَّنَاءَ بِحَمْدِكَ

**Ewe Mungu wangu! Hakika mimi naanza kukutukuza
kwa hamdi Yako,**

وَأنتَ مُسَدِّدٌ لِلصَّوَابِ بِمَنِّكَ

**Nawe ni Mwenye kuelekeza kwenye usahihi kwa
wema Wako.**

وَأَيَّقِنْتُ أَنَّكَ أَنْتَ أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ فِي مَوْضِعِ العَفْوِ
وَالرَّحْمَةِ

Nina yakini kuwa hakika Wewe ndiye Mbora wa warehemevu pale panapostahiki msamaha na rehema.

وَأَشَدُّ الْمُعَاقِبِينَ فِي مَوْضِعِ النَّكَالِ وَالنَّقْمَةِ

Lakini ni mkali wa adhabu pale panapostahiki onyo na adhabu.

وَأَعْظَمُ الْمُتَجَبِّرِينَ فِي مَوْضِعِ الْكِبْرِيَاءِ وَالْعِظْمَةِ

Na ni mwenye nguvu kuliko majabari pale panapostahiki kiburi na nguvu.

اللَّهُمَّ أَذِنْتَ لِي فِي دُعَائِكَ وَمَسْأَلَتِكَ

Ewe Mungu wangu! Umenipa idhini ya kusoma dua na kukuomba,

فَاسْمَعْ يَا سَمِيعَ مِدْحَتِي

Hivyo sikiliza utukuzo wangu ewe Msikivu!

وَأَجِبْ يَا رَحِيمَ دَعْوَتِي

Nijibu ombi langu ewe Mrehemevu!

وَأَقِلْ يَا غَفُورُ عَثْرَتِي

Samehe makosa yangu ewe Msamehevu!

فَكَمْ يَا إِلَهِي مِنْ كُرْبَةٍ قَدْ فَرَّجْتَهَا

Matatizo mangapi ewe Mungu wangu umeyafariji,

وَهُمُومٌ قَدْ كَشَفْتَهَا

Na tabu ngapi umeziiondoa,

وَعَثْرَةٍ قَدْ أَقْلَتَهَا

Makosa mangapi umeyaondoa,

وَرَحْمَةٍ قَدْ نَشَرْتَهَا

Rehema ngapi umezieneza,

وَحَلَقَةٍ بَلَاءٍ قَدْ فَكَّكْتَهَا

Na milolongo mingapi ya balaa umeitawanya.

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي لَمْ يَتَّخِذْ صَاحِبَةً وَلَا وُلْدًا

**Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu ambaye hana
mke wala mtoto.**

وَلَمْ يَكُنْ لَهُ شَرِيكٌ فِي الْمُلْكِ

Hana mshirika katika ufalme,

وَلَمْ يَكُنْ لَهُ وَلِيٌّ مِنَ الذُّلِّ وَكَبَّرَهُ تَكْبِيرًا

Hana msaidizi kwa udhalili, hivyo mtukuze mno.

الْحَمْدُ لِلَّهِ بِجَمِيعِ مَحَامِدِهِ كُلِّهَا عَلَى جَمِيعِ نِعَمِهِ كُلِّهَا

Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu kwa yote anayostahili kusifiwa juu ya neema Zake zote.

الْحَمْدُ لِلَّهِ لَا مُضَادَّ لَهُ فِي مُلْكِهِ وَلَا مُنَازِعَ لَهُ فِي أَمْرِهِ

Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu asiye na mkabala katika ufalme Wake, wala mpinzani katika amri Yake.

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي لَا شَرِيكَ لَهُ فِي خَلْقِهِ وَلَا شَبِيهَ لَهُ فِي عَظَمَتِهِ

Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu ambaye hana mshirika katika kuumba Kwake, wala mwenza katika utukufu Wake.

الْحَمْدُ لِلَّهِ الْفَاشِي فِي الْخَلْقِ امْرُهُ وَحَمْدُهُ

Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu mwenye kueneza miongozo kwa viumbe.

الظَّاهِرِ بِالْكَرَمِ مَجْدُهُ

**Na utukufu wake uko dhahiri kwa uzuri wa ukarimu
Wake.**

الْبَاسِطِ بِالْجُودِ يَدُهُ

Mwenye kufumbua mkono Wake kwa ukarimu Wake.

الَّذِي لَا تَنْقُصُ خَزَائِنُهُ

Ambaye hazina Yake haipunguki.

وَلَا تَزِيدُهُ كَثْرَةُ الْعَطَاءِ إِلَّا جُودًا وَكَرَمًا

Wala wingi wa utoaji hauzidishi ila ukarimu.

إِنَّهُ هُوَ الْعَزِيزُ الْوَهَّابُ

Hakika Yeye ni Mwenye uwezo na Mtoaji.

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ قَلِيلًا مِنْ كَثِيرٍ

**Ewe Mungu wangu! Hakika mimi nakuomba
kichache toka kwenye kingi,**

مَعَ حَاجَةٍ بِي إِلَيْهِ عَظِيمَةٍ

Japokuwa haja yangu kwacho ni kubwa.

وَعِنَّاكَ عَنْهُ قَدِيمٌ وَهُوَ عِنْدِي كَثِيرٌ

Na kutokukihitaji Kwako ni kwa kudumu, nacho kwangu ni kingi,

وَهُوَ عَلَيْكَ سَهْلٌ يَسِيرٌ

Na kwako ni chepesi na rahisi.

اللَّهُمَّ إِنَّ عَفْوَكَ عَنْ ذَنْبِي

Ewe Mungu wangu! Hakika msamaha wako wa dhambi zangu,

وَتَجَاوَزَكَ عَنْ خَطِيئَتِي

Na usamehevu Wako makosa yangu,

وَصَفْحَكَ عَنْ ظُلْمِي

Usamehevu Wako wa dhulma yangu,

وَسِتْرِكَ عَلَى قَبِيحِ عَمَلِي

Na sitara Yako juu ya ubaya wa amali yangu,

وَحِلْمِكَ عَنْ كَثِيرِ جُرْهِي

Na upole Wako dhidi ya wingi wa makosa yangu,

عِنْدَ مَا كَانَ مِنْ خَطَايِي وَعَمْدِي

Pindi nikukoseapo kwa bahati mbaya na makusudi,

أَطْمَعَنِي فِي أَنْ أَسْأَلَكَ مَا لَا أَسْتَوْجِبُهُ مِنْكَ

Yamenitamanisha nikuombe yale nisiyopaswa kutoka kwako.

الَّذِي رَزَقْتَنِي مِنْ رَحْمَتِكَ

Ambayo umeniruzuku toka kwenye rehema Zako,

وَأَرَيْتَنِي مِنْ قُدْرَتِكَ

Na umenionyesha toka kwenye uwezo Wako,

وَعَرَّفْتَنِي مِنْ إِجَابَتِكَ

Na umenitambulisha toka kwenye majibu Yako.

فَصِرْتُ أَدْعُوكَ آمِنًا

**Hivyo nimekuwa nikikuita huku nikiwa ni mwenye
amani,**

وَأَسْأَلُكَ مُسْتَأْنِسًا

Na nikukuomba huku nikiwa sina upweke.

لَا خَائِفًا وَلَا وَجِلًا

Sina khofu wala woga,

مُدًّا لَكَ عَلَيَّ فِيمَا قَصَدْتُ فِيهِ إِلَيْكَ

**Bali nina imani juu Yako kuhusu yale niliyokusudia
Kwako.**

فَإِنَّ أِبْطَأَ عَنِّي عَتَبْتُ بِجَهْلِي عَلَيْكَ

**Likawiyapo (jibu) hukulalamikia kwa ujinga wangu
juu Yako,**

وَلَعَلَّ الَّذِي أِبْطَأَ عَنِّي هُوَ خَيْرٌ لِي

**Na huenda ulilolikawiza kwa ajili yangu ndio kheri
kwangu.**

لَعَلِمِكَ بِعَاقِبَةِ الْأُمُورِ

**Kwa kuwa Wewe ndiye Mjuzi wa matokeo ya
baadaye.**

فَلَمْ أَرَ مَوْلَىٰ كَرِيمًا أَصْبَرَ عَلَىٰ عَبْدٍ لِّئِيمٍ مِنْكَ عَلَيَّ

**Sijamwona bwana mkarimu mwenye kumvumilia mja
muovu kushinda Wewe ulivyo juu yangu.**

يَا رَبِّي إِنَّكَ تَدْعُونِي فَأَوْلِي عَنكَ

**Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika wewe waniita, nami
nakukimbia.**

وَتَتَحَبَّبُ إِلَيَّ وَآتَبَغَّضُ إِلَيْكَ

**Unaonyesha huba kwangu, nami naonyesha chuki
kwako.**

وَتَتَوَدَّدُ إِلَيَّ فَلَا أَقْبَلُ مِنْكَ

Unaonyesha mapenzi kwa ajili yangu lakini sikubali,

كَأَنَّ لِي التَّطَوُّلَ عَلَيْكَ

Kana kwamba nina nguvu juu Yako.

فَلَمْ يَمْنَعَكَ ذَلِكَ مِنَ الرَّحْمَةِ لِي

Lakini hayo yote hayajakuzuia kunipa rehema Zako

وَالْإِحْسَانَ إِلَيَّ

Na ihsani Yako.

وَالْتَفَضُّلِ عَلَيَّ بِجُودِكَ وَكَرَمِكَ

Wala kunifanyia fadhila kwa ukarimu wako na wema Wako.

فَارْحَمْ عَبْدَكَ الْجَاهِلَ

Basi mrehemu mja Wako mjinga.

وَجِدْ عَلَيْهِ بِفَضْلِ إِحْسَانِكَ

Mkirimu kwa fadhila za ihsani Yako.

إِنَّكَ جَوَادٌ كَرِيمٌ

Hakika Wewe ni Mkarimu, Mwema.

الْحَمْدُ لِلَّهِ مَالِكِ الْمَلِكِ مُجْرِي الْفُلْكِ

Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu, Mmiliki wa ufalme, Mwendeshaji wa meli,

مُسَخَّرِ الرِّيحِ فَالِقِ الْأَصْبَاحِ

Mpelekaji wa pepo, Mletaji wa machweo,

دَيَّانِ الدِّينِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

Mamlaka ya siku ya malipo na Mola Mlezi wa viumbe.

الْحَمْدُ لِلَّهِ عَلَى حِلْمِهِ بَعْدَ عِلْمِهِ

Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu kwa ustahmilivu Wake baada ya elimu Yake.

وَ الْحَمْدُ لِلَّهِ عَلَى عَفْوِهِ بَعْدَ قُدْرَتِهِ

Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu kwa msamaha Wake baada ya uwezo Wake.

وَ الْحَمْدُ لِلَّهِ عَلَى طَوْلِ أَنَاتِهِ فِي غَضَبِهِ

Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu kwa urefu wa subira Yake anapoghadhibika,

وَهُوَ قَادِرٌ عَلَى مَا يُرِيدُ

Na Yeye ni Mwenye uwezo juu ya lile alitakalo.

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ خَالِقِ الْخَلْقِ

Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu Muumba wa viumbe,

بَاسِطِ الرِّزْقِ فَالِقِ الْإِصْبَاحِ

Mtoaji wa riziki, Mletaji wa machweo,

ذِي الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ

Mwenye utukufu na heshima,

وَالْفَضْلِ وَالْإِنْعَامِ

Mwenye fadhila na neema.

الَّذِي بَعْدَ فَلَا يُرَى

Ambaye kajiweka mbali hawezi kuonekana,

وَقَرُبَ فَشَهِدَ النَّجْوَى

Ambaye yu karibu ashuhudia siri.

تَبَارَكَ وَتَعَالَى

Ametakasika na kutukuka jina Lake.

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي لَيْسَ لَهُ مُنَازِعٌ يُعَادِلُهُ

Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu, ambaye hana mpinzani anayelingana naye,

وَلَا شَبِيهٌ يُشَاكِلُهُ

Wala shabihi wa namna Yake,

وَلَا ظَهِيرٌ يُعَاوِدُهُ

Wala msaidizi ampaye nguvu.

قَهَرَ بِعِزَّتِهِ الْأَعْزَاءَ

Kwa nguvu Zake kuwatenza nguvu wababe,

وَتَوَاضَعَ لِعِظْمَتِهِ الْعُظَمَاءَ

Na kwa utukufu Wake wamenyenyekea wakuu.

فَبَلِّغْ بِقُدْرَتِهِ مَا يَشَاءُ

Hivyo kwa uwezo Wake akayafikia ayatakayo.

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي يُجِيبُنِي حِينَ أُنَادِيهِ

**Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu, ambaye
hunijibu nimwitapo,**

وَيَسْتُرْ عَلَيَّ كُلَّ عَوْرَةٍ وَأَنَا أَعْصِيهِ

Husitiri kila aibu yangu ilihali mimi namuasi,

وَيُعْظِمُ النِّعْمَةَ عَلَيَّ فَلَا أُجَازِيهِ

Huongeza neema kwangu na wala simlipi.

فَكَمْ مِنْ مَوْهَبَةٍ هَنِيئَةٍ قَدْ أَعْطَانِي

Kwani ni hiba ngapi tulivu amenipa.

وَعَظِيمَةٍ مَخُوفَةٍ قَدْ كَفَانِي

Ni makubwa mangapi ya kukhofisha ameniondolea.

وَبَهْجَةٍ مُنْقَدَةٍ قَدْ آرَانِي

Ni furaha ngapi changamfu amenionyesha.

فَأُثْنِي عَلَيْهِ حَامِداً

Hivyo namtukuza kwa kumsifu,

وَأَذْكُرُهُ مُسَبِّحًا

Na ninamtaja kwa kumsabihi.

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي لَا يَهْتَكُ حِجَابَهُ

**Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu, ambaye pazia
Yake hairaruriwi.**

وَلَا يُغْلَقُ بَابُهُ وَلَا يُرَدُّ سَائِلُهُ

**Wala mlango Wake haufungwi, Wala muombaji
Kwake hanyimwi.**

وَلَا يُخَيِّبُ آمِلُهُ

Wala matumaini yake hayafelishwi.

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي يُؤْمِنُ الْخَائِفِينَ

**Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu, ambaye
huwapa amani wenye hofu.**

وَيُنَجِّي الصَّالِحِينَ

Huwaokoa waja wema.

وَيَرْفَعُ الْمُسْتَضْعَفِينَ

Huwanyanyua waliodhoofishwa.

وَيَضَعُ الْمُسْتَكْبِرِينَ

Huwafedhehesha wenye viburi.

وَيُهْلِكُ مُلُوكًا وَيَسْتَخْلِفُ آخَرِينَ

**Huwaangamiza wafalme, na (sehemu zao) huwaweka
wengine.**

وَ الْحَمْدُ لِلَّهِ قَاصِمِ الْجَبَّارِينَ

**Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu. Mwenye
kuwafutilia mbali majabari,**

مُبِيرِ الظَّالِمِينَ

Mwenye kuwaangamiza madhalimu,

مُدْرِكِ الْهَارِيْنَ

Mwenye kuwafikia wanaomkimbia,

نَكَالِ الظَّالِمِينَ

Mtoa adhabu kwa madhalimu,

صَرِيحِ الْمُسْتَصْرِحِينَ

**Msaidizi wa wenye kulia kwa ukelele wakiomba
msaada.**

مَوْضِعِ حَاجَاتِ الطَّالِبِينَ

Na kwake yeye ndiko kwenye mahitaji ya watafutaji,

مُعْتَمِدِ الْمُؤْمِنِينَ

Na Yeye ndiye tegemeo la waumini.

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي مِنْ خَشْيَتِهِ تَرَعَدُ السَّمَاوُ وَتَسْكَاثُنَا

Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu, Ambaye kwa kumwogopa Yeye mbingu na wakazi wake hutikisika,

وَتَرَجُفُ الْأَرْضُ وَعَمَّارُهَا

Na milima na wakazi wake hugwaya,

وَتَمُوجُ الْبَحَارُ وَمَنْ يَسْبَحُ فِي غَمَرَاتِهَا

Na bahari hufanya mawimbi ikiwa na waogeleaji wake.

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي هَدَانَا لِهَذَا وَمَا كُنَّا لِنَهْتَدِيَ لَوْلَا أَنْ هَدَانَا اللَّهُ

Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu, Ambaye ametuongoza kwenye hili, na tusingeweza kuongoka lau Mwenyezi Mungu asingetuongoza.

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي يَخْلُقُ وَلَمْ يَخْلُقْ

Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu, Ambaye huumba na hajaumbwa,

وَيَرْزُقُ وَلَا يُرْزَقُ

Huruzuku na wala hapewi riziki,

وَيُطْعَمُ وَلَا يُطْعَمُ

Hulisha na wala halishwi,

وَيَمِيتُ الْأَحْيَاءَ

Huwafisha walio hai,

وَيُحْيِي الْمَوْتَى

Huwapa uhai walio wafu,

وَهُوَ حَيٌّ لَا يَمُوتُ

Yeye ni hai asiyekufa,

بِيَدِهِ الْخَيْرُ

Kheri iko mkononi mwake.

وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

Na Yeye ni Muweza wa kila kitu.

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ

Ewe Mungu wangu! Mrehemu Muhammad.

عَبْدِكَ وَرَسُولِكَ

Mja Wako na Mtume Wako,

وَأَمِينِكَ وَصَفِيِّكَ وَحَبِيبِكَ

Mwaminifu Kwako, mteule Wako na hababi Wako,

وَخَيْرَتِكَ مَنْ خَلَقَكَ

Chaguo Lako bora kati ya viumbe Wako,

وَحَافِظِ سِرِّكَ وَمُبَلِّغِ رِسَالَتِكَ

**Muhifadhi wa siri Yako na mfikishaji wa ujumbe
Wako,**

أَفْضَلَ وَأَحْسَنَ وَأَجْمَلَ وَأَكْمَلَ

**Aliye mbora zaidi, mwema zaidi, mzuri mno,
mkamilifu zaidi,**

وَأَزْكِي وَأَنْعَى وَأَطْيَبَ وَأَطْهَرَ وَأَسْنَى وَأَكْثَرَ

Takasifu zaidi, itukuzwayo zaidi, tukufu mno na safi mno,

مَا صَلَّيْتَ وَبَارَكْتَ وَتَرَحَّمْتَ وَتَحَنَّنْتَ وَسَلَّمْتَ عَلَى
أَحَدٍ مِّنْ عِبَادِكَ وَأَنْبِيَائِكَ وَرُسُلِكَ وَصِفْوَتِكَ وَأَهْلِ
الْكَرَامَةِ عَلَيْكَ مِنْ خَلْقِكَ

Kushinda ile uliyemrehemu, kumbariki, kumhurumia na kumtakia rehema yeyote miongoni mwa waja Wako, Manabii Wako, Mitume Wako, wateule Wako na wenyewe heshima Kwako miongoni mwa viumbe Wako.

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى عَلِيِّ أَمِيرِ الْمُؤْمِنِينَ

Ewe Mungu wangu! Mrehemu Ali Jemedari wa Waumini,

وَوَصِيِّ رَسُولِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

Wasii wa Mtume wa Mola Mlezi wa viumbe.

عَبْدِكَ وَوَلِيِّكَ

Mja Wako na kipenzi Chako.

وَأَخِي رَسُولِكَ وَحُجَّتِكَ عَلَى خَلْقِكَ

**Binamu wa Mtume Wako na hoja Yako juu ya viumbe
Wako.**

وَأَيَّتِكَ الْكُبْرَى وَالنَّبَأَ الْعَظِيمِ

Alama Yako kubwa na habari kuu.

وَصَلِّيَّ عَلَى الصِّدِّيقَةِ الطَّاهِرَةِ

Na mrehemu mkweli, mtoharifu,

فَاطِمَةَ الزَّهْرَاءِ سَيِّدَةَ نِسَاءِ الْعَالَمِينَ

**Fatima Zahra, Bibi mbora kushinda wanawake wote
wa ulimwengu.**

وَصَلِّيَّ عَلَى سِبْطِي الرَّحْمَةِ

Warehemu wajukuu wawili wa rehema,

وَأَمَامَايِ الْهُدَى

Na maimamu wa uongofu,

الْحَسَنَ وَالْحُسَيْنَ سَيِّدَيِ شَبَابِ أَهْلِ الْجَنَّةِ

Hasan na Husein, Mabwana wawili wa vijana wa Peponi.

وَصَلِّيْ عَلَيَّ عَلَى أُمَّةِ الْمُسْلِمِيْنَ ،

Warehemu maimamu wa waislamu:

عَلِيِّ بْنِ الْحُسَيْنِ

Ali bin Husein,

وَمُحَمَّدِ بْنِ عَلِيٍّ

Muhammad bin Ali,

وَجَعْفَرِ بْنِ مُحَمَّدٍ

Jafar bin Muhammad,

وَمُوسَى بْنِ جَعْفَرٍ

Musa bin Jafar,

وَعَلِيِّ بْنِ مُوسَى

Ali bin Musa,

وَمُحَمَّدِ بْنِ عَلِيٍّ

Muhammad bin Ali,

وَعَلِيِّ بْنِ مُحَمَّدٍ

Ali bin Muhammad,

وَالْحَسَنِ بْنِ عَلِيٍّ

Hasan bin Ali,

وَالْخَلْفِ الْهَادِي الْمَهْدِيِّ

mrithi na mwongozaji, Mahdi

حُجَّتِكَ عَلَى عِبَادِكَ

Hoja Wako juu ya waja Wako,

وَأَمْنَائِكَ فِي بِلَادِكَ

Na waaminifu katika nchi Yako.

صَلَوَةً كَثِيرَةً دَائِمَةً

Warehemu rehema nyingi za kudumu.

اللَّهُمَّ وَصِّلِي عَلَى وَلِيِّ أَمْرِكَ

**Ewe Mungu wangu! Mrehemu mwangalizi wa jambo
Lako,**

الْقَائِمِ الْمُؤَمَّلِ

Mwakilishi mwenye kutarajiwa,

وَالْعَدْلِ الْمُنْتَظَرِ

Na mwadilifu mwenye kungojewa.

وَحُفِّهِ بِمَلَائِكَتِكَ الْمُقَرَّبِينَ

Mzungushie Malaika Wako walio wa karibu,

وَأَيِّدْهُ بِرُوحِ الْقُدُسِ

Msaidie kwa Raho mtakatifu,

يَا رَبَّ الْعَالَمِينَ

Ewe Mola Mlezi wa viumbe.

اللَّهُمَّ اجْعَلْهُ الدَّاعِيَ إِلَىٰ كِتَابِكَ

**Ewe Mungu wangu! Mfanye awe mlinganizi kwenye
Kitabu Chako,**

وَالْقَائِمَ بِدِينِكَ

Na msimamizi wa dini Yako,

اسْتَخْلَفَهُ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفْتَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِ

**Mfanye Khalifa ardhini kama ulivyowafanya
makhalifa wale wa kabla yake.**

مَكِّنْ لَهُ دِينَهُ الَّذِي ارْتَضَيْتَهُ

Mwimarishie dini yake uliyoiridhia.

أَبْدِلْهُ مِنْ بَعْدِ خَوْفِهِ أَمْنًا

Mpe amani baada ya khofu.

يَعْبُدُكَ لَا يُشْرِكُ بِكَ شَيْئًا

Akuabudu bila kukushirikisha na chochote.

اللَّهُمَّ أَعِزَّهُ وَأَعِزِّ بِهِ

**Ewe Mungu wangu! Mpe nguvu na kupitia yeye wape
wengine nguvu,**

وَأَنْصُرُهُ وَأَنْتَصِرْ بِهِ

Msaidie na kupitia yeye wasaidie wengine.

وَأَنْصُرُهُ نَصْرًا عَزِيزًا

Msaidie msaada uliotukuka.

وَأَفْتَحْ لَهُ فَتْحًا يَسِيرًا

Mpe ushindi kirahisi.

وَأَجْعَلْ لَهُ مِنْ لَدُنْكَ سُلْطَانًا نَصِيرًا

Mpe mamlaka saidizi kutoka Kwako.

اللَّهُمَّ أَظْهِرْ بِهِ دِينَكَ وَسُنَّةَ نَبِيِّكَ

**Ewe Mungu wangu! Kupitia yeye idhihirishe dini
Yako na Sunna ya Nabii Wako,**

حَتَّى لَا يَسْتَخْفِيَ بِشَيْءٍ مِنْ الْحَقِّ مَخَافَةَ أَحَدٍ مِّنَ
الْخَلْقِ

**Mpaka sehemu yoyote ya haki isifichikane kwa
kumwogopa yeyoye kati ya viumbe.**

اللَّهُمَّ إِنَّا نَرْغَبُ إِلَيْكَ فِي دَوْلَةٍ كَرِيمَةٍ

**Ewe Mungu wangu! Hakika sisi tuna hamu mno na
dola ya heshima toka Kwako,**

تُعِزُّ بِهَا الْإِسْلَامَ وَأَهْلَهُ

Ambayo kwayo Uislamu na watu wake utapata nguvu,

وَتُذِلُّ بِهَا النِّفَاقَ وَأَهْلَهُ

Na unafiki na watu wake utadhalilika.

وَتَجْعَلُنَا فِيهَا مِنَ الدُّعَاةِ إِلَى طَاعَتِكَ

Utujalie humo tuwe walinganizi kwenye utii Wako,

وَالْقَادَةِ إِلَى سَبِيلِكَ

Na viongozi kwenye njia Yako.

وَتَرَزُّقُنَا بِهَا كَرَامَةَ الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ

Uturuzuku kwayo heshima ya Dunia na Akhera.

اللَّهُمَّ مَا عَرَّفْتَنَا مِنَ الْحَقِّ فَحَمِّلْنَاهُ

**Ewe Mungu wangu! Haki uliyotuelimisha tusaidie
tuitekeleze,**

وَمَا قَصْرُنَا عَنْهُ فَبَلِّغْنَاهُ

Na tuliyoipuuzia tujaalie tuifikie.

اللَّهُمَّ أَلِّمْنَا بِهِنَّ شَعْنَنَا وَاشْعَبْ بِهِنَّ صَدْعَنَا

**Ewe Mungu wangu! Kupitia yeye tusuluhishie mambo
yetu na unganisha makundi yetu.**

وَارْتُقْ بِهِنَّ فَتَقْنَا وَكَثِّرْ بِهِنَّ قَلْتَنَا

**Weka pamoja mtengano wetu na kithirisha uchache
wetu.**

وَأَعِزُّ بِهِنَّ ذِلَّتَنَا وَاعْنِ بِهِنَّ عَائِلَنَا

Upe heshima udhalili wetu na tajirisha familia zetu.

وَاقْضِ بِهِ عَنْ مَغْرَمِنَا وَاجْبُرْ بِهِ فَقْرَنَا

Mlipie deni mdaiwa wetu na ondoa ufakiri wetu.

وَسُدِّ بِهِ خَلَّتْنَا وَيَسِّرْ بِهِ عُسْرَنَا

Ziba pengo la mahitaji yetu na rahisisha mazito yetu.

وَبَيِّضْ بِهِ وُجُوهُنَا وَفُكِّ بِهِ أَسْرَنَا

Zing'arisha nyoyo zetu na wape uhuru mateka wetu.

وَأَنْجِحْ بِهِ طَلَبَتْنَا وَأَنْجِزْ بِهِ مَوَاعِيدِنَا

Tufanikishie maombi yetu na tutimizie ahadi yetu.

وَاسْتَجِبْ بِهِ دَعْوَتَنَا وَأَعْطِنَا بِهِ سُؤْلَنَا

Tujibu dua yetu na tupe maombi yetu.

وَبَلِّغْنَا بِهِ مِنَ الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ آمَالَنَا

Tutimizie matarajio yetu duniani na Akhera.

وَأَعْطِنَا بِهِ فَوْقَ رَغْبَتِنَا

Na utupe zaidi ya mategemeo yetu.

يَا خَيْرَ الْمَسْئُولِينَ وَأَوْسَعَ الْمُعْطِينَ

Ewe mbora wa waombwaji na mkuu wa watoaji.

إشْفِ بِهِ صُدُورَنَا وَأَذْهِبْ بِهِ غَيْظَ قُلُوبِنَا

Kupitia yeye viponye vifua vyetu na ondoa vinyongo vya nyoyo zetu,

وَاهْدِنَا بِهِ لِمَا اخْتَلَفَ فِيهِ مِنَ الْحَقِّ بِإِذْنِكَ

Tuongoze kwa idhini Yako kwenye haki waliyotofautiana,

إِنَّكَ تَهْدِي مَنْ تَشَاءُ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ

Hakika wewe humwongoza umtakaye kwenye njia nyoofu.

وَأَنْصُرْنَا بِهِ عَلَى عَدُوِّكَ وَعَدُونَا

Na kupitia yeye tusaidie dhidi ya adui Wako na adui wetu.

إِلَهَ الْحَقِّ آمِينَ

Ewe Mungu wa haki, amin.

اللَّهُمَّ إِنَّا نَشْكُو إِلَيْكَ فَقَدْ نَبَّيْنَا صَلَوَاتِكَ عَلَيْهِ وَآلِهِ

**Ewe Mungu wangu! Hakika sisi tunakushtakia
kutoweka kwa Mtume wetu, rehema
Zako ziwe juu yake na juu ya kizazi chake,**

وَعَيْبَةَ وَلِيِّنَا وَكَثْرَةَ عَدُوِّنَا

ghaiba ya walii wetu na uwingi wa maadui zetu,

وَقِلَّةَ عَدَدِنَا وَشِدَّةَ الْفِتَنِ بِنَا

uchache wa idadi yetu na ukali wa fitina kwetu,

وَتَظَاهُرَ الزَّمَانِ عَلَيْنَا

na ushindi wa zama dhidi yetu.

فَصَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ

Hivyo mrehemu Muhammad na kizazi chake,

وَأَعِنَّا عَلَى ذَلِكَ بِفَتْحٍ مِنْكَ تُعَجِّلُهُ

**Na tusaidie katika hilo kwa ushindi wa haraka toka
Kwako.**

وَبِضْرٍ تَكْشِفُهُ

Na kwa kutuondolea madhara,

وَنَصْرٍ تُعِزُّهُ

Kwa msaada uupao nguvu,

وَسُلْطَانٍ حَقِّ تَظْهِرُهُ

Kwa mamlaka ya haki uidhihirishayo,

وَرَحْمَةٍ مِنْكَ تُجَلِّلُنَاهَا

Kwa rehema utupazo heshima kwazo toka Kwako,

وَعَافِيَةٍ مِنْكَ تُلْبِسُنَاهَا

Na kwa afya utuvalishayo toka Kwako.

بِرَحْمَتِكَ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ

Kwa rehema Zako ewe mbora wa warehemevu.

DUA YA TANO

Dua hii inazungumzia starehe za Peponi na adhabu za ndani ya Jahannam. Kuamini juu ya Akhera ndio mzizi wa mwisho muhimu wa dini na Dua hii ni ufuatiliaji unaostahili wa Dua al-Iftitah ambayo inazungumzia juu ya misingi mingine ya Imani.

Thawabu na mateso yanayowangojea wanadamu yanaelezwa kwa kinaganaga kwa ajili ya muumini kuweza kuyabaini hayo. Haitoshi tu kibusara kuamini juu ya Akhera. Kama vile tu inavyopendekezwa mtu kujifikiria anavyokufa ili aweze kujiandaa kwa kifo kwa uhakika, ni muhimu vilevile kujifikiria mtu kwamba yuko Peponi au Jahannam kwa ajili ya uimarishaji wa imani juu ya Akhera.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa kurehemu.

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ

Ewe Mungu wangu! Mrehemu Muhammad, na Aali Muhammad.

اللَّهُمَّ بِرَحْمَتِكَ فِي الصَّالِحِينَ فَأَدْخِلْنَا

Ewe Mungu wangu! Kwa rehema Zako tujumuishe na wachamungu.

وَفِي عَلَيْنَ فَاَرْفَعْنَا

Tunyanyue tuwe pamoja na wenye heshima.

وَبِكَاسٍ مِنْ مَعِينٍ مِنْ عَيْنٍ سَلَسَبِيلٍ فَاسْقِنَا

Tunyweshe kwa kikombe cha maji toka chemchem ya Salsabili.

وَمِنَ الْحُورِ الْعِينِ بِرَحْمَتِكَ فَزَوِّجْنَا

Kwa rehema Zako tuozeshe hurulaini.

وَمِنَ الْوُلْدَانِ الْمُخَلَّدِينَ كَأَنَّهُمْ لَوْلُو مَكْنُونٌ فَآخِذِمْنَا

Tupe wahudumu miongoni mwa wavulana wasiochakaa walio kama lulu zilizofichwa.

وَمِنْ ثَمَارِ الْجَنَّةِ وَلِحُومِ الطَّيْرِ فَاطْعِمْنَا

Tulishe matunda ya Peponi na nyama za ndege.

وَمِنْ ثِيَابِ السُّنْدُسِ وَالْحَرِيرِ وَالْإِسْتَبْرَقِ فَالْبَسْنَا

Na tuvishie nguo za hariri nzito na laini.

وَلَيْلَةَ الْقَدْرِ وَحَجَّ بَيْتِكَ الْحَرَامِ

**Tuwafikishe tuipate Laylatul-Qadri, Tuhiji nyumba
Yako tukufu.**

وَقْتَلًا فِي سَبِيلِكَ فَوْقَ لَنَا

Tuuwawe katika njia Yako.

وَصَالِحِ الدُّعَاءِ وَالْمَسْئَلَةِ فَاسْتَجِبْ لَنَا

Na utujibu dua na maombi mema.

وَإِذَا جَمَعْتَ الْأُولَيْنِ وَالْآخِرِينَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فَارْحَمْنَا

**Uturehemu utakapowakusanya wa zamani na wa
mwisho siku ya Kiyama.**

وَبَرَاءَةً مِنَ النَّارِ فَاكْتُبْ لَنَا

Tuandikie tuepukane na moto.

وَفِي جَهَنَّمَ فَلَا تَغْلُنَا

Usituzamishe ndani ya Jahannam.

وَفِي عَذَابِكَ وَهَوَانِكَ فَلَا تَبْتَلِنَا

Na usitujaribu ndani ya adhabu Yako na udhalili Wako.

وَمِنَ الزَّقُّومِ وَالضَّرِّعِ فَلَا تُطْعِمْنَا

Usitulishe mti wa Zaquum wala wa Dharii.

وَمَعَ الشَّيَاطِينِ فَلَا تَجْعَلْنَا

Usituweke pamoja na mashetani.

وَفِي النَّارِ عَلَى وُجُوهِنَا فَلَا تَكْبُبْنَا

Usiziangushie nyuso zetu juu ya moto.

وَمِن ثِيَابِ النَّارِ وَسَرَابِيلِ الْقَطْرَانِ فَلَا تُلْبِسْنَا

Usituvishie nguo za moto na kanzu zenye lami.

وَمِن كُلِّ سُوءٍ

Na kila kwenye baya tuepushe.

يَا لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ

Ewe Ambaye hapana Mungu wa haki ila Wewe.

بِحَقِّ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ فَانجِنَا

Tuokoe kwa utukufu wa tamko ‘hapana Mungu wa haki ila Wewe’.

DUA YA SITA

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.**

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ

**Ewe Mungu wangu! Mrehemu Muhammad na Aali za
Muhammad.**

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ أَنْ تَجْعَلَ لِي فِي مَا تَقْضِي وَتُقَدِّرُ

**Ewe Mungu wangu! Hakika mimi nakuomba uweke
katika yale unayopitisha na kukadiria,**

مِنَ الْأَمْرِ الْمُحْتُمِّ فِي الْأَمْرِ الْحَكِيمِ

Miongoni mwa mambo ya uhakika yenye hekima,

مِنَ الْقَضَاءِ الَّذِي لَا يُرَدُّ وَلَا يُبَدَّلُ

Toka kwenye pitisho lisilokataliwa wala kubadilishwa.

أَنْ تَكْتُبَنِي مِنْ حُجَّاجِ بَيْتِكَ الْحَرَامِ

**Uniandike miongoni mwa mahujaji wa nyumba Yako
tukufu,**

الْمَبْرُورِ حَجُّهُمْ الْمَشْكُورِ سَعِيهِمْ

**Ambao Hijja yao imekubaliwa, juhudi zao zimeth-
aminiwa,**

الْمَغْفُورِ ذُنُوبِهِمْ الْمَكْفَرِ عَنْ سَيِّئَاتِهِمْ

**Dhambi zao wamesamehewa na makosa yao yamefut-
wa.**

وَأَنْ تَجْعَلَ فِيمَا تَقْضِي وَتُقَدِّرُ

Na uweke katika yale unayopitisha na kukadiria,

أَنْ تُطِيلَ عُمْرِي فِي خَيْرٍ وَعَافِيَةٍ

Kwamba umri wangu urefuke katika kheri na afya,

وَتُوسِّعَ فِي رِزْقِي

Na riziki yangu ipanuke.

وَتَجْعَلَنِي مِمَّنْ تَنْتَصِرُ بِهِ لِذِينِكَ

**Niweke miongoni mwa wale ambao, kupitia kwao
unaipa ushindi Dini Yako.**

وَلَا تَسْتَبْدِلْ بِي غَيْرِي

Na wala usimweke mwingine badala yangu.

يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ

Ewe mbora wa Warehemevu.

DUA YA SABA

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.**

أَعُوذُ بِجَلَالِ وَجْهِكَ الْكَرِيمِ

Najikinga kupitia utukufu wa heshima Yako kuu,

أَنْ يَنْقُضِي عَنِّي شَهْرَ رَمَضَانَ

Usimalizike mwezi wa Ramadhani,

أَوْ يَطَّلِعَ الْفَجْرُ مِنْ لَيْلِي هَذِهِ

Au kuchomoza alfajiri ya usiku wangu huu,

وَلَكَ قِبَلِي تَبَعَةٌ أَوْ ذَنْبٌ تُعَذِّبُنِي عَلَيْهِ

**Na wewe Kwangu una la kufuatilia au dhambi
utakayoniadhibu kwa ajili yake.**

DUA YA SAHRI (DAKU)

Hii ni Dua moja nzuri sana. Lugha yake ya kishairi na ujumbe wake unaogusa moyo unafanya iwe ni Dua nzuri sana. Rehema ya Mwenyezi Mungu inayozunguka kila kitu inafananishwa na ukubwa mpana sana wa bahari, ambapo wenye haja na shida ni wasafiri katika meli wakingojea kuvuka.

Unyenyekevu ni sehemu muhimu sana ya taratibu na adabu za Dua.

Utambuzi wa dhambi zake mtu na mapungufu mengine kunafaa sana kwa muombaji. Hili linaelezwa kwa ufupi na uwazi katika Dua ifuatayo:

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.**

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ

**Ewe Mwenyezi Mungu! Mrehemu Muhammad na
Aali Muhammad.**

إِلَهِي وَقَفَ السَّائِلُونَ بِبَابِكَ

**Ewe Mungu wangu! Waombaji wamesimama
mlangoni Kwako.**

وَلَاذَ الْفُقَرَاءِ بِجَنَابِكَ

Mafukara wamekimbilia kwenye heshima Yako.

وَوَقَفْتُ سَفِينَةَ الْمَسَاكِينِ عَلَى سَاحِلِ بَحْرِ جُودِكَ
وَكَرَمِكَ

Safina ya masikini imesimama kwenye mwambao wa bahari ya ukarimu Wako na wema wako.

يَرْجُونَ الْجَوَازَ إِلَى سَاحَةِ رَحْمَتِكَ وَنِعْمَتِكَ

Wanataraji kuvuka kwenda kwenye uwanja wa rehema Zako na neema Zako.

إِلَهِي إِنْ كُنْتَ لَا تَرْحَمُ فِي هَذَا الشَّهْرِ الشَّرِيفِ إِلَّا
لِمَنْ أَخْلَصَ لَكَ فِي صِيَامِهِ وَقِيَامِهِ

Ewe Mungu wangu! Ukiwa humhurumii ndani ya mwezi huu mtukufu ila mwenye ikhlasi kwako katika funga yake na Swala yake,

فَمَنْ لِلْمُذْنِبِ الْمُقْصِرِ إِذَا غَرِقَ فِي بَحْرِ ذُنُوبِهِ وَأَثَامِهِ

Basi ni nani atamhurumia mwenye dhambi mzembe anapozama kwenye bahari ya dhambi zake na makosa yake!?

إِلَهِي إِنْ كُنْتَ لَا تَرْحَمُ إِلَّا الْمُطِيعِينَ فَمَنْ لِلْعَاصِينَ

**Ewe Mola wangu! Ukiwa huwahurumii ila watiifu,
basi ni nani atawahurumia waasi!?**

وَإِنْ كُنْتَ لَا تَقْبَلُ إِلَّا مِنَ الْعَامِلِينَ، فَمَنْ لِلْمُقَصِّرِينَ

**Na ukiwa hupokei ila kutoka kwa wenye matendo mazuri,
Basi ni nani atawahurumia wenye kuzembea!?**

إِلَهِي رِيحَ الصَّائِمُونَ

Ewe Mungu wangu! Wenye Swaumu wamefaulu,

وَفَارَ الْقَائِمُونَ وَنَجَى الْمُخْلِصُونَ،

**Wenye kusimama kwa ajili ya Swala wamefuzu, Na
wenye ikhlaswi wameokoka.**

وَنَحْنُ عِبِيدُكَ الْمَذْنِبُونَ

Na sisi ni waja Wako wenye dhambi,

فَارْحَمْنَا بِرَحْمَتِكَ

Hivyo turehemu kwa rehema Zako.

وَاعْتِقْنَا مِنَ النَّارِ بِعَفْوِكَ يَا كَرِيمُ

Na tutoe motoni kwa msamaha Wako ewe Mkarimu.

يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ

Ewe mbora wa Warehemevu.

وَصَلَّى اللَّهُ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ الطَّاهِرِينَ

Na mrehemu Muhammad na Aali zake watoharifu.

ZIYARA AL-WARITHA

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا وَارِثَ آدَمَ صَفْوَةَ اللَّهِ

**Amani iwe juu yako ewe mrithi wa Adam mteule wa
Mwenyezi Mungu!**

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا وَارِثَ نُوحِ نَبِيِّ اللَّهِ

**Amani iwe juu yako ewe mrithi wa Nuh Nabii wa
Mwenyezi Mungu!**

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا وَارِثَ إِبْرَاهِيمَ خَلِيلِ اللَّهِ

**Amani iwe juu yako ewe mrithi wa Ibrahim kipenzi
cha Mwenyezi Mungu!**

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا وَارِثَ مُوسَى كَلِيمِ اللَّهِ

**Amani iwe juu yako ewe mrithi wa Musa aliyesema na
Mwenyezi Mungu!**

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا وَارِثَ عِيسَى رُوحِ اللَّهِ

**Amani iwe juu yako ewe mrithi wa Isa roho wa
Mwenyezi Mungu!**

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا وَارِثَ مُحَمَّدٍ حَبِيبِ اللَّهِ

**Amani iwe juu yako ewe mrithi wa Muhammad
kipenzi cha Mwenyezi Mungu!**

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا وَارِثَ أَمِيرِ الْمُؤْمِنِينَ وَوَلِيِّ اللَّهِ

**Amani iwe juu yako ewe mrithi wa Jemedari wa
Waumini walii wa Mwenyezi Mungu!**

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بَنَ مُحَمَّدٍ الْمُصْطَفَى

**Amani iwe juu yako ewe mwana wa Muhammad
Al-Mustafa!**

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بَنَ عَلِيِّ الْمُرْتَضَى

Amani iwe juu yako ewe mwana wa Ali Al-Murtadha!

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بَنَ فَاطِمَةَ الزَّهْرَاءِ

Amani iwe juu yako ewe mwana wa Fatima Zahraa!

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بَنَ خَدِيجَةَ الْكُبْرَى

**Amani iwe juu yako ewe mwana wa Khadija
Al-Kubra!**

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا ثَارَ اللَّهِ وَابْنَ ثَارِهِ وَالْوَثَرَ الْمُؤْتُورَ

Amani iwe juu yako ewe ambaye kisasi chake kitalipizwa na Mwenyezi Mungu. Na mwana wa ambaye kisasi chake kitalipizwa na yeye! Na aliye wa pekee kwake.

أَشْهَدُ أَنَّكَ قَدْ أَقَمْتَ الصَّلَاةَ وَأَتَيْتَ الزَّكَاةَ

Nakiri kuwa hakika wewe umesimamisha Swala na umetoa Zaka.

وَأَمَرْتَ بِالْمَعْرُوفِ وَنَهَيْتَ عَنِ الْمُنْكَرِ

Umeamrisha mema na kukataza mabaya.

وَأَطَعْتَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ حَتَّىٰ آتَاكَ الْيَقِينَ

Na umemtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake mpaka yakini ilipokufika.

فَلَعَنَ اللَّهُ أُمَّةً قَتَلَتْكَ

Mwenyezi Mungu aulani umma uliokuua.

وَلَعَنَ اللَّهُ أُمَّةً ظَلَمْتَكَ

Mwenyezi Mungu aulani umma uliokudhulumu.

وَلَعَنَّ اللَّهُ أُمَّةً سَمِعَتْ بِذَلِكَ فَرَضِيَتْ بِهِ

Mwenyezi Mungu aulani umma uliosikia hayo kisha ukayaridhia.

يَا مَوْلَايَ يَا أَبَا عَبْدِ اللَّهِ

Ewe bwana wangu! Ewe Abu Abdillah!

أَشْهَدُ أَنَّكَ كُنْتَ نُورًا فِي الْأَصْلَابِ الشَّامِخَةِ
وَالْأَرْحَامِ الْمُطَهَّرَةِ

Nakiri kuwa hakika wewe ulikuwa nuru kwenye mifupa ya migongo ya juu na matumbo ya uzazi yaliyo tohara.

لَمْ تُنَجِّسْكَ الْجَاهِلِيَّةُ بِأَنْجَاسِهَا

Ujahiliya haujakuchafua kwa uchafu wake.

وَلَمْ تُلِيسْكَ مِنْ مُدْلِهِمَاتِ ثِيَابِهَا

Wala giza halikukufunika kwa shuka lake.

وَأَشْهَدُ أَنَّكَ مِنْ دَعَائِمِ الدِّينِ وَأَرْكَانِ الْمُؤْمِنِينَ

Nakiri kuwa hakika wewe unatokana na nguzo za dini na viongozi wa waumini.

وَأَشْهَدُ أَنَّكَ الْإِمَامُ الْبَرُّ التَّقِيُّ الرَّضِيُّ

**Nakiri kuwa hakika wewe ni Imam mwema,
mchamungu mwenye kuridhiwa.**

الزَّكِيُّ الْهَادِي الْمَهْدِيُّ

Mtakasifu, kiongozi muongozaji kwa haki.

وَأَشْهَدُ أَنَّ الْأَيْمَةَ مِنْ وُلْدِكَ كَلِمَةُ التَّقْوَى

**Nakiri kuwa hakika Maimamu toka kwenye kizazi
chako ni neno la uchamungu,**

وَأَعْلَامُ الْهُدَى وَالْعُرْوَةُ الْوُثْقَى

Alama za uongofu, shikio imara,

وَالْحُجَّةُ عَلَى أَهْلِ الدُّنْيَا

Na hoja juu ya watu wa duniani.

وَأَشْهَدُ اللَّهَ وَمَلَائِكَتَهُ وَأَنْبِيَائَهُ وَرُسُلَهُ

**Namshuhudisha Mwenyezi Mungu na malaika Wake,
Manabii Wake na Mitume Wake,**

أَنْتِ بِكُمْ مُؤْمِنٌ وَيَايَابِكُمْ

Kuwa hakika mimi ni mwenye kuwaamini nyinyi, na ni mwenye yakini na kurudi kwenu,

مُوقِنٌ بِشَرَائِعِ دِينِي وَخَوَاتِيمِ عَمَلِي

Sheria za dini yangu, na matokeo ya matendo yangu.

وَقَلْبِي لِقَلْبِكُمْ سَلَمٌ

Moyo wangu ni wenye kujisalimisha kwenye nyoyo zenu.

وَأَمْرِي لِأَمْرِكُمْ مُتَّبِعٌ

Na mambo yangu ni yenye kufuata mambo yenu.

صَلَوَاتُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ

Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yenu,

وَعَلَى أَرْوَاحِكُمْ وَعَلَى أَجْسَادِكُمْ وَعَلَى أَجْسَامِكُمْ

Na juu ya roho zenu, miili yenu, na viwiliwili vyenu.

وَعَلَى شَاهِدِكُمْ وَعَلَى غَائِبِكُمْ

Juu ya anayeonekana na asiyeonekana,

وَعَلَى ظَاهِرِكُمْ وَعَلَى بَاطِنِكُمْ

Aliye dhahiri na asiye dhahiri.

ZIYARA YA ALI AKBAR (A.S.)

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بَنَ رَسُولِ اللَّهِ

**Amani iwe juu yako ewe mwana wa Mtume wa
Mwenyezi Mungu!**

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بَنَ نَبِيِّ اللَّهِ

**Amani iwe juu yako ewe mwana wa Nabii wa
Mwenyezi Mungu!**

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بَنَ أَمِيرِ الْمُؤْمِنِينَ

**Amani iwe juu yako ewe mwana wa Jemedari wa
Waumini!**

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بَنَ الْحُسَيْنِ الشَّهِيدِ

Amani iwe juu yako ewe mwana wa Husein shahidi!

السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا الشَّهِيدُ وَابْنَ الشَّهِيدِ

Amani iwe juu yako ewe shahidi na mwana wa shahidi!

السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا الْمَظْلُومُ وَابْنَ الْمَظْلُومِ

Amani iwe juu yako ewe uliyedhulumiwa mwana wa aliyedhulumiwa!

لَعَنَ اللَّهُ أُمَّةً قَتَلَتْكَ

Mwenyezi Mungu aulani umma uliokuua.

وَلَعَنَ اللَّهُ أُمَّةً ظَلَمَتْكَ

Mwenyezi Mungu aulani umma uliokudhulumu.

وَلَعَنَ اللَّهُ أُمَّةً سَمِعَتْ بِذَلِكَ فَرَضِيَتْ بِهِ

Mwenyezi Mungu aulani umma uliosikia hayo kisha ukayaridhia.

ZIYARA YA WAHANGA WOTE

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا أَوْلِيَاءَ اللَّهِ وَآحِبَّائِهِ

Amani iwe juu yenu enyi mawalii wa Mwenyezi Mungu na vipenzi Vyake!

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا أَصْفِيَاءَ اللَّهِ وَأَوْدَاءَهُ

**Amani iwe juu yenu enyi wateule wa Mwenyezi
Mungu na vipenzi Vyake!**

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا أَنْصَارَ دِينِ اللَّهِ

**Amani iwe juu yenu enyi wasaidizi wa dini ya
Mwenyezi Mungu!**

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا أَنْصَارَ رَسُولِ اللَّهِ

**Amani iwe juu yenu enyi wasaidizi wa Mtume wa
Mwenyezi Mungu!**

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا أَنْصَارَ أَمِيرِ الْمُؤْمِنِينَ

**Amani iwe juu yenu enyi wasaidizi wa Jemedari wa
Waumini!**

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا أَنْصَارَ فَاطِمَةَ الزَّهْرَاءِ سَيِّدَةِ
نِسَاءِ الْعَالَمِينَ

**Amani iwe juu yenu enyi wasaidizi wa Fatima, Bibi
mbora kushinda wanawake wote wa ulimwengu!**

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا أَنْصَارَ أَبِي مُحَمَّدٍ الْحَسَنِ بْنِ عَلِيٍّ
الْوَلِيِّ النَّاصِحِ

**Amani iwe juu yenu enyi wasaidizi wa Abu Muham-
mad Hasan ibnu Ali, walii mtakasifu na mnasihi!**

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا أَنْصَارَ أَبِي عَبْدِ اللَّهِ

Amani iwe juu yenu enyi wasaidizi wa Abu Abdillah!

بِأَبِي أَنْتُمْ وَأُمِّي

Baba yangu na mama yangu ni fidia kwenu.

طَبِئْتُمْ وَطَابَتِ الْأَرْضُ الَّتِي فِيهَا دُفِنْتُمْ

Hakika mmesafika na imesafika ardhi mliyozikwa.

وَفُزْتُمْ فَوْزاً عَظِيماً

Na mmefuza kufuzu kukubwa mno.

فِيَا لَيْتَنِي كُنْتُ مَعَكُمْ فَأَفُوزَ مَعَكُمْ

**Natamani laiti ningelikuwa pamoja nanyi nikafuzu
pamoja nanyi.**

ZIYARA YA ABUL-FADHLI ABBAS (A.S.)

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا أَبَا الْفَضْلِ الْعَبَّاسَ ابْنَ أَمِيرِ
الْمُؤْمِنِينَ

**Amani iwe juu yako ewe Abul-Fadhli Abbas! Mwana
wa Jemedari wa Waumini!**

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا ابْنَ سَيِّدِ الْوَصِيِّينَ

Amani iwe juu yako ewe mwana wa bwana wa mawasii!

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا ابْنَ أَوَّلِ الْقَوْمِ إِسْلَامًا وَ أَوَّلِ قَدَمِهِمْ
إِيمَانًا

**Amani iwe juu yako ewe mwana wa wa kwanza kuwa
mwisilamu, na wa mwanzo kuamini.**

وَ أَقْوَمِهِمْ بِدِينِ اللَّهِ وَ أَحْوَطِهِمْ عَلَى الْإِسْلَامِ

**Aliye imara mno kwenye dini ya Mwenyezi Mungu na
mjuzi mno juu ya Uisilamu.**

أَشْهَدُ لَقَدْ نَصَحْتَ لِلَّهِ وَ لِرِسُولِهِ وَ لِأَخِيكَ

**Nakiri kuwa umetoa nasaha kwa ajili ya Mwenyezi
Mungu, Mtume Wake na kaka yako.**

فَنِعَمَ الْأَخُ الْمُوَاسِي

Ni uzuri ulioje kwa wewe kuwa ndugu mfariji!

فَلَعَنَ اللَّهُ أُمَّةً قَتَلَتْكَ

Mwenyezi Mungu aulani umma uliokuuwa.

وَلَعَنَ اللَّهُ أُمَّةً ظَلَمَتْكَ

Mwenyezi Mungu aulani umma uliokudhulumu.

وَلَعَنَ اللَّهُ أُمَّةً اسْتَحَلَّتْ مِنْكَ الْمَحَارِمَ

**Mwenyezi Mungu aulani umma uliohalalisha haramu
dhidi yako,**

وَانتَهَكْتَ حُرْمَةَ الْإِسْلَامِ

Na ukavunja heshima ya Uisilamu.

فَنِعَمَ الصَّابِرُ الْمُجَاهِدُ الْمُحَامِي النَّاصِرُ

**Ni uzuri ulioje kwa wewe kuwa mvumilivu,
Mpiganaji, muhami na msaidizi,**

وَ الْأَخِ الدَّافِعُ عَنْ أَخِيهِ الْمُجِيبُ إِلَى طَاعَةِ رَبِّهِ

Ndugu mtetezi kwa ndugu yake na mtiifu kwa Mola wake,

الرَّاعِبُ فِيمَا زَهَدَ فِيهِ غَيْرُهُ

Mwenye kupendelea yale waliyoyapa mgongo wengine,

مِنَ الثَّوَابِ الْجَزِيلِ وَ الثَّنَاءِ الْجَمِيلِ

Kuanzia thawabu njema hadi sifa jamili.

وَ أَلْحَقَكَ (فَأَلْحَقَكَ) اللَّهُ بِدَرَجَةِ آبَائِكَ فِي جَنَاتِ
النَّعِيمِ

Mwenyezi Mungu akuweke kwenye daraja la baba zako ndani ya pepo yenye neema.

DUA BAADA YA ZIYARA

اللَّهُمَّ إِنِّي تَعَرَّضْتُ لِزِيَارَةِ أَوْلِيَائِكَ رَغْبَةً فِي ثَوَابِكَ

Ewe Mungu wangu! Nimekusudia mwenyewe kuwazuru mawalii Wako kwa ajili ya kutamani thawabu Zako.

وَرَجَاءَ لِمَغْفِرَتِكَ وَ جَزِيلِ إِحْسَانِكَ

Na kutaraji msamaha Wako na ihsani Yako njema.

فَأَسْأَلُكَ أَنْ تُصَلِّيَ عَلَيَّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَ آلِهِ الطَّاهِرِينَ

Hivyo nakuomba mrehemu Muhammad na Aali zake watoharifu.

وَ أَنْ تَجْعَلَ رِزْقِي بِهِمْ دَارًا

Na kupitia kwao ifanye maridhawa riziki yangu.

وَ عَيْشِي بِهِمْ قَارًا

Fanya maisha yangu yawe yenye kupendeza.

وَ زِيَارَتِي بِهِمْ مَقْبُولَةً

Ziyara yangu ikubalike.

وَ حَيَاتِي بِهِمْ طَيِّبَةً

Na maisha yangu yawe ya kufurahisha.

وَ أَدْرِجْنِي إِدْرَاجَ الْمُكْرَمِينَ

Niweke pamoja na wale wenye kuheshimiwa.

وَاجْعَلْنِي مِمَّنْ يَنْقَلِبُ مِنْ زِيَارَةِ مَشَاهِدِ أَحِبَّائِكَ

**Nijalie niwe miongoni mwa wale wanaorudi toka kuzuru
makaburi ya wapenzi Wako,**

مُفْلِحاً مُنْجِحاً

Huku wakiwa ni wenye kufaulu na kufuzu.

قَدْ اسْتُوجِبَ غُفْرَانَ الذُّنُوبِ

Ambao wamewajibika kusamehewa dhambi,

وَ سَتَرَ الْعُيُوبِ وَ كَشَفَ الْكُرُوبِ

Kusitiriwa aibu na kuondolewa matatizo.

إِنَّكَ أَهْلُ التَّقْوَى وَ أَهْلُ الْمَغْفِرَةِ .

Hakika Wewe ni mwenye kupokea uchamungu na kumiliki msamaha.

DUA ZA KILA SIKU YA RAMADHANI

MWEZI MOSI:

اللَّهُمَّ اجْعَلْ صِيَامِي فِيهِ صِيَامَ الصَّائِمِينَ

Ewe Mungu wangu! Ijalie funga yangu katika mwezi huu iwe ni funga ya wenye kufunga kwa dhati.

وَقِيَامِي فِيهِ قِيَامَ الْقَائِمِينَ

Na kisimamo changu cha ibada kiwe ni kisimamo cha wenye kusimama kwa ibada ya dhati.

وَنَبِّئِي فِيهِ عَن نُّومَةِ الْغَافِلِينَ

Niepushe na usingizi wa wavivu,

وَهَبْ لِي جُرْمِي فِيهِ يَا إِلَهَ الْعَالَمِينَ

Samehe dhambi zangu humo ewe Mola wa viumbe.

وَاعْفُ عَنِّي يَا عَافِيًا عَنِ الْمُجْرِمِينَ

Na uniafu ewe mwenye kuwasamehe wakosaji.

MWEZI PILI:

اللَّهُمَّ قَرِّبْنِي فِيهِ إِلَى مَرْضَاتِكَ

**Ewe Mungu wangu! Nikurubishe kwenye radhi ndani
ya mwezi huu.**

وَجَبِّبْنِي فِيهِ مِنْ سَخَطِكَ وَنِقَمَاتِكَ

**Niepushe na hasira Zako na maangamizo Yako ndani
ya mwezi huu.**

وَوَفِّقْنِي فِيهِ لِقِرَاءَةِ آيَاتِكَ

Na uniwafikishe niweze kukisoma Kitabu Chako.

بِرَحْمَتِكَ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ

Kwa rehema Zako ewe mbora wa warehemevu.

MWEZI TATU:

اللَّهُمَّ ارْزُقْنِي فِيهِ الذِّهْنَ وَالتَّنْبِيْهَ

Ewe Mungu wangu! Niruzuku uelevu na uzinduko,

وَبَاعِدْنِي فِيهِ مِنَ السَّفَاهَةِ وَالتَّمْوِينِ

Niepushe na ubaradhuli na upumbavu,

وَأَجْعَلْ لِي نَصِيباً مِنْ كُلِّ خَيْرٍ تُنَزَّلُ فِيهِ

Na niwezeshe kupata fungu la kila kheri itakayoshuka,

بِجُودِكَ يَا أَجُودَ الْأَجُودِينَ

Kwa ukarimu Wako ewe mbora wa wakarimu.

MWEZI NNE:

اللَّهُمَّ قَوِّنِي فِيهِ عَلَى إِقَامَةِ أَمْرِكَ

Ewe Mungu wangu! Nipe nguvu za kuniwezesha
kutekeleza amri Zako.

وَأَذِقْنِي فِيهِ حَلَاوَةَ ذِكْرِكَ

Nionjeshe humu utamu wa utajo Wako.

وَأَوْزِعْنِي فِيهِ لِأَدَاءِ شُكْرِكَ بِكَرَمِكَ

Niwezeshe kutekeleza wajibu wa kukushukuru kwa
neema Zako.

وَاحْفَظْنِي فِيهِ بِحِفْظِكَ وَسَتْرِكَ

Na nihifadhi humu katika ulinzi Wako na sitara Yako.

يَا أَبْصَرَ النَّاطِرِينَ

Ewe mwenye kuona zaidi ya waoni.

MWEZI TANO:

اللَّهُمَّ اجْعَلْنِي فِيهِ مِنَ الْمُسْتَغْفِرِينَ

Ewe Mungu wangu! Nijalie ndani ya mwezi huu niwe miongoni mwa wanaoomba maghofira.

وَاجْعَلْنِي فِيهِ مِنْ عِبَادِكَ الصَّالِحِينَ الْقَانِتِينَ

Nijalie niwe miongoni mwa waja Wako wema wanyenyekevu.

وَاجْعَلْنِي فِيهِ مِنْ أَوْلِيَائِكَ الْمُقَرَّبِينَ

Na nijaalie niwe miongoni mwa mawalii Wako wa karibu.

بِرَأْفَتِكَ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ

Kwa huruma Yako ewe mbora wa wenye huruma.

MWEZI SITA:

اللَّهُمَّ لَا تَخْذُلْنِي فِيهِ لِتَعَرُّضِ مَعْصِيَتِكَ

Ewe Mungu wangu! Usinitelekeze kwa kukuasi.

وَلَا تَضْرِبْنِي بِسَيِّئِ نَقِمَتِكَ

Wala usinipige kwa mjeledi wa adhabu Yako.

وَزَحْزَحْنِي فِيهِ مِنْ مُوجِبَاتِ سَخَطِكَ

**Niepushe na mambo yote yawezayo kuniwajibishia
hasira Zako.**

بِمَنَّكَ وَأَيَادِيكَ يَا مُنْتَهَى رَغْبَةِ الرَّاعِبِينَ

**Kwa ukarimu Wako na baraka Zako ewe uliye raghba
ya wenye raghba.**

MWEZI SABA:

اللَّهُمَّ أَعِنِّي فِيهِ عَلَى صِيَامِهِ وَقِيَامِهِ

**Ewe Mungu wangu! Nisaidie niweze kuufunga na
kusimama kwa ajili ya ibada.**

وَجَنِّبْنِي فِيهِ مِنْ هَفَوَاتِهِ وَأَثَامِهِ

Niepushe na matelezo na madhambi.

وَارْزُقْنِي فِيهِ ذِكْرَكَ بِدَوَامِهِ

Na niruzuku nidumu katika utajo Wako.

بِتَوْفِيقِكَ يَا هَادِيَ الْمُضِلِّينَ

Kwa tawfiki Yako ewe Mwongozaji wa waliopotea.

MWEZI NANE:

اللَّهُمَّ ارْزُقْنِي فِيهِ رَحْمَةَ الْأَيْتَامِ

**Ewe Mungu wangu! Niruzuku hali ya kuwaonea
huruma mayatima,**

وَإِطْعَامِ الطَّعَامِ وَإِفْشَاءِ السَّلَامِ

**Kulisha vyakula, kutoa salamu, na kusuhubiana na
watu wema.**

وَصُحْبَةِ الْكِرَامِ يَا مَلْجَأَ الْأَمَلِينَ

Kwa utajiri Wako ewe kimbilio la wenye matarajio.

MWEZI TISA:

اللَّهُمَّ اجْعَلْ لِي فِيهِ نَصِيباً مِنْ رَحْمَتِكَ الْوَاسِعَةِ

**Ewe Mungu wangu! Nijalie nilipate fungu la rehema
Zako pana.**

وَاهِدِنِي فِيهِ لِبِرَاهِينِكَ السَّاطِعَةِ

Uniongoze kwenye buruhani Zako zing'arazo.

وَخُذْ بِنَاصِيَّتِي إِلَى مَرْضَاتِكَ الْجَامِعَةِ

Na nishike mkono kuelekea kwenye radhi Zako kuu.

بِمَحَبَّتِكَ يَا أَمَلَ الْمُشْتَاقِينَ

**Kwa mahaba Yako ewe uliye matarajio ya wenye
shauku.**

MWEZI KUMI:

اللَّهُمَّ اجْعَلْنِي فِيهِ مِنَ الْمُتَوَكِّلِينَ عَلَيْكَ

**Ewe Mungu wangu! Nijalie niwe miongoni mwa
wenye kukutegemea.**

وَاجْعَلْنِي فِيهِ مِنَ الْفَائِزِينَ لَدَيْكَ

Nijalie niwe miongoni mwa wenye kufuzu mbele Yako.

وَاجْعَلْنِي فِيهِ مِنَ الْمُقْرَبِينَ إِلَيْكَ

**Na nijalie niwe miongoni mwa wenye ukuruba
Kwako.**

بِإِحْسَانِكَ يَا غَايَةَ الطَّالِبِينَ

Kwa ihsani Yako ewe uliye lengo la waombaji.

MWEZI KUMI NA MOJA:

اللَّهُمَّ حَبِّبْ إِلَيَّ فِيهِ الْإِحْسَانَ

**Ewe Mungu wangu! Nijalie nipende sana kutenda
mema.**

وَكْرَهُ إِلَيَّ فِيهِ الْفُسُوقَ وَالْعِصْيَانَ

Na niwezeshe kuchukia kutenda uovu na uasi.

وَحَرِّمْ عَلَيَّ فِيهِ السَّخَطَ وَالنِّيْرَانَ

Na niepushe na hasira Zako na moto.

بِعَوْنِكَ يَا غِيَاثَ الْمُسْتَغِيثِينَ

Kwa msaada Wako ewe uliye nusra ya watakao nusra.

MWEZI KUMI NA MBILI:

اللَّهُمَّ زَيِّنِي فِيهِ بِالسِّتْرِ وَالْعَفَافِ

Ewe Mungu wangu! Nipambe kwa sitara na utawa.

وَاسْتُرْنِي فِيهِ بِلِبَاسِ الْقُنُوعِ وَالْعَفَافِ

Nipambe kwa vazi la ukinaifu na utoshekevu.

وَاحْمَلْنِي فِيهِ عَلَى الْعَدْلِ وَالْإِنْصَافِ

Nielekeze kwenye uadilifu na insafu.

وَأَمِّئِي فِيهِ مِنْ كُلِّ مَا أَخَافُ

Na nisalimisha dhidi ya kila ninachohofia.

بِعِصْمَتِكَ يَا عِصْمَةَ الْخَائِفِينَ

Kwa kinga Yako ewe uliye kinga ya wenye hofu.

MWEZI KUMI NA TATU:

اللَّهُمَّ طَهِّرْنِي فِيهِ مِنَ الدَّنَسِ وَالْأَقْدَارِ

Ewe Mungu wangu! Nitakase dhidi ya taka na uchafu.

وَصَبِّرْنِي فِيهِ عَلَى كَائِنَاتِ الْأَقْدَارِ

Nipe subira juu ya matukio ya kadari Zako.

وَوَفِّقْنِي فِيهِ لِلتَّقَى وَصُحْبَةِ الْأَبْرَارِ

Na niafikishe kwenye uchaji na kusuhubiana na watu wema.

بِعَوْنِكَ يَا قُرَّةَ عَيْنِ الْمَسَاكِينِ

Kwa msaada Wako ewe kiburudisho cha walio masikini.

MWEZI KUMI NA NNE:

اللَّهُمَّ لَا تُؤَاخِذْنِي فِيهِ بِالْعَثَرَاتِ

Ewe Mungu wangu! Usinihakumu kwa yale niliyojikwaa.

وَأَقْلِنِي فِيهِ مِنَ الْخَطَايَا وَالْهَفَوَاتِ

Niepushe na makosa na matelezo.

وَلَا تَجْعَلْنِي فِيهِ غَرَضًا لِلْبَلَايَا وَالْآفَاتِ

Na wala usinifanye shabaha la balaa na maafa.

بِعِزَّتِكَ يَا عِزُّ الْمُسْلِمِينَ

Kwa utukufu Wako ewe uliye utukufu wa Waislamu.

MWEZI KUMI NA TANO:

اللَّهُمَّ ارْزُقْنِي فِيهِ طَاعَةَ الْخَاشِعِينَ

Ewe Mungu wangu! Niruzuku utiifu wa wenye unyenyekevu.

وَأَسْرَحْ فِيهِ صَدْرِي بِإِنَابَةِ الْمُخْبِتِينَ

Na kikunjue kifua changu kwa toba ya wenye kujisalimisha.

بِأَمَانِكَ يَا أَمَانَ الْخَائِفِينَ

Kwa amani Yako ewe uliye amani ya wenye hofu.

MWEZI KUMI NA SITA:

اللَّهُمَّ وَقِّفْنِي فِيهِ لِمُؤَافَقَةِ الْأَبْرَارِ

Ewe Mungu wangu! Niafikishe niafikiane na watu wema.

وَجَنِّبْنِي فِيهِ مُرَافَقَةَ الْأَشْرَارِ

Niepushe kurafikiana na waovu.

وَأُونِي فِيهِ بِرَحْمَتِكَ إِلَى دَارِ الْقَرَارِ

Na uniweke kwa rehema Zako kwenye nyumba ya utulivu.

بِالْمَهِيَّتِكَ يَا إِلَهَ الْعَالَمِينَ

Kwa utukufu Wako ewe Mungu! wa viumbe.

MWEZI KUMI NA SABA:

اللَّهُمَّ اهْدِنِي فِيهِ لِمُصَالِحِ الْأَعْمَالِ

Ewe Mungu wangu! Niongoze kwenye amali njema.

وَاقْضِ لِي فِيهِ الْحَوَائِجَ وَالْأَمَالَ

Na nitekelezee haja zangu na matarajio yangu.

يَا مَنْ لَا يَحْتَاجُ إِلَى التَّفْسِيرِ وَالسُّوَالِ

Ewe usiyehitaji ufafanuzi na kuuliza.

يَا عَالِماً بِمَا فِي صُدُورِ الْعَالَمِينَ

Ewe Mjuzi wa yale yaliyomo vifuani mwa viumbe.

صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ الطَّاهِرِينَ

Mrehemu Muhammad na Aali zake watoharifu.

MWEZI KUMI NA NANE:

اللَّهُمَّ نَبِّهْنِي فِيهِ لِبَرَكَاتِ أَسْحَارِهِ

Ewe Mungu wangu! Nizindue ili nipate baraka za masiku yake.

وَنَوِّزْ فِيهِ قَلْبِي بِضِيَاءِ أَنْوَارِهِ

Ung'arisha moyo wangu kwa mwangaza wa nuru zake.

وَحُذِّ بِكُلِّ أَعْضَائِي إِلَى اتِّبَاعِ آثَارِهِ

Na vishike mkono viungo vyangu vyote vifuate athari zake.

بِنُورِكَ يَا مُنَوَّرَ قُلُوبِ الْعَارِفِينَ

Kwa nuru Yako ewe Mwangazi wa nyoyo za wakujuao.

MWEZI KUMI NA TISA:

اللَّهُمَّ وَفِّرْ فِيهِ حَظِّي مِنْ بَرَكَاتِهِ

Ewe Mungu wangu! Niongezee fungu langu la baraka za mwezi huu.

وَسَهِّلْ سَبِيلِي إِلَى خَيْرَاتِهِ

Nisahilishie njia ya kuzifikia kheri zake.

وَلَا تَحْرِمْنِي قَبُولَ حَسَنَاتِهِ

Wala usininyime kabuli ya mema yake.

يَا هَادِيًا إِلَى الْحَقِّ الْمُبِينِ

Ewe uongozaye kwenye haki iliyo wazi.

MWEZI ISHIRINI:

اللَّهُمَّ افْتَحْ لِي فِيهِ أَبْوَابَ الْجَنَانِ

Ewe Mungu wangu! Nifungulie milango ya Peponi.

وَأَغْلِقْ عَنِّي فِيهِ أَبْوَابَ النَّيِّرَانِ

Unifungie milango ya moto.

وَوَقِّفْنِي فِيهِ لِتِلَاوَةِ الْقُرْآنِ

Na niafikishe niweze kuisoma Qur'an.

يَا مُنْزِلَ السَّكِينَةِ فِي قُلُوبِ الْمُؤْمِنِينَ

Ewe Mwenye kutia utulivu nyoyoni mwa waumini.

MWEZI ISHIRINI NA MOJA:

اللَّهُمَّ اجْعَلْ لِي فِيهِ إِلَى مَرْضَاتِكَ دَلِيلًا

Ewe Mungu wangu! Niwekee mwongozo wa kufikia radhi Zako.

وَلَا تَجْعَلْ لِلشَّيْطَانِ فِيهِ عَلَيَّ سَبِيلًا

Usimpe shetani nafasi juu yangu.

وَاجْعَلِ الْجَنَّةَ لِي مَنزِلًا وَمَقِيلًا

Na ifanye Pepo iwe ndiyo mashukio yangu na mapumziko.

يَا قَاضِيَ حَوَائِجِ الطَّالِبِينَ

Ewe mwenye kukidhi haja za wakuombao.

MWEZI ISHIRINI NA MBILI:

اللَّهُمَّ افْتَحْ لِي فِيهِ أَبْوَابَ فَضْلِكَ

Ewe Mungu wangu! Nifungulie milango ya fadhila Zako.

وَأَنْزِلْ عَلَيَّ فِيهِ بَرَكَاتِكَ

Niteremshie baraka Zako.

وَوَفِّقْنِي فِيهِ لِمُوجِبَاتِ مَرْضَاتِكَ

Niafikishe nitende viwajibishi vya radhi Zako.

وَأَسْكِنِّي فِيهِ بِحُبُوحَاتِ جَنَّاتِكَ

Na unipe makazi kwenye maliwazo ya Pepo Yako.

يَا مُجِيبَ دَعْوَةِ الْمُضْطَرِّينَ

Ewe Mwitika wa maombi ya wenye dhiki.

MWEZI ISHIRINI NA TATU:

اللَّهُمَّ اغْسِلْنِي فِيهِ مِنَ الذُّنُوبِ

Ewe Mungu wangu! Nisafishe dhidi ya madhambi.

وَطَهِّرْنِي فِيهِ مِنَ الْعُيُوبِ

Nitakase na aibu.

وَأَمْتَحِنْ قَلْبِي فِيهِ بِتَقْوَى الْقُلُوبِ

Na uonjeshe moyo wangu uchaji wa kweli.

يَا مُقِيلَ عَثَرَاتِ الْمَذْنِبِينَ

Ewe Msamehevu wa matelezo ya wenye dhambi.

MWEZI ISHIRINI NA NNE:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ فِيهِ مَا يُرْضِيكَ

**Ewe Mungu wangu! Nakuomba yale
yanayokuridhisha.**

وَأَعُوذُ بِكَ مِمَّا يُؤْذِيكَ

Na ninajikinga Kwako na yale yanayokuudhi.

وَأَسْأَلُكَ التَّوْفِيقَ فِيهِ لِأَنْ أَطِيعَكَ وَلَا أَعْصِيكَ

Na ninakuomba uniwafikishe niweze kukutii na wala nisikuasi.

يَا جَوَادَ السَّائِلِينَ

Ewe uliye mkarimu kwa waombao.

MWEZI ISHIRINI NA TANO:

اللَّهُمَّ اجْعَلْنِي فِيهِ مُحِبًّا لِأَوْلِيَائِكَ

Ewe Mungu wangu! Nijalie niwe mwenye kuwapenda mawalii Wako.

وَمُعَادِيًّا لِأَعْدَائِكَ

Mwenye kuwachukia maadui Zako.

مُسْتَنًّا بِسُنَّةِ خَاتِمِ أَنْبِيَائِكَ

Na mwenye kufuata mwenendo wa hitimisho la Mitume Wako.

يَا عَاصِمَ قُلُوبِ النَّبِيِّينَ

Ewe mwenye kuzitakasa nyoyo za Mitume.

MWEZI ISHIRINI NA SITA:

اللَّهُمَّ اجْعَلْ سَعْيِي فِيهِ مَشْكُورًا

Ewe Mungu wangu! Jalia juhudi zangu ziwe ni zenye kuthaminiwa.

وَذَنْبِي فِيهِ مَغْفُورًا

Dhambi zangu ziwe ni zenye kusamehewa.

وَعَمَلِي فِيهِ مَقْبُولًا

Na amali zangu ziwe ni zenye kukubaliwa.

وَعَيْبِي فِيهِ مَسْتُورًا

Na aibu zangu ziwe ni zenye kusitiriwa.

يَا أَسْمَعَ السَّمْعِينَ

Ewe Mbora wa wasikivu.

MWEZI ISHIRINI NA SABA:

اللَّهُمَّ ارْزُقْنِي فِيهِ فَضْلَ لَيْلَةِ الْقَدْرِ

Ewe Mungu wangu! Niruzuku fadhila za usiku wa Laylatul-Qadri.

وَصَيِّرْ أُمُورِي فِيهِ مِنْ الْعُسْرِ إِلَى الْيُسْرِ

Humo uyageuze mambo yangu mazito yawe mepesi.

وَأَقْبَلْ مَعَاذِيرِي

Zikubali nyudhuru zangu.

وَحُطِّ عَنِّي الذَّنْبَ وَالْوِزْرَ

Na uniondolee mzigo wa dhambi.

يَا رَوْفًا بَعْبَادِهِ الصَّالِحِينَ

Ewe uliye Mpole kwa waja wema.

MWEZI ISHIRINI NA NANE:

اللَّهُمَّ وَفِّرْ حَظِّي فِيهِ مِنَ النَّوَافِلِ

Ewe Mungu wangu! Niongezee fungu langu la ibada za ziada ndani ya mwezi huu.

وَأَكْرَمْنِي فِيهِ بِأَحْضَارِ الْمَسَائِلِ

Nikirimu kwa kuweza kuhudhurisha maombi.

وَقَرَّبْ فِيهِ وَسَيْلَتِي إِلَيْكَ مِنْ بَيْنِ الْوَسَائِلِ

Nisogezee njia miongoni mwa njia za kukufikia.

يَا مَنْ لَا يَشْغُلُهُ الْحَاحُ الْمَلْحِينِ

Ewe Ambaye hushughulishwi na mahimizo ya wahimizao.

MWEZI ISHIRINI NA TISA:

اللَّهُمَّ غَشِّنِي فِيهِ بِالرَّحْمَةِ

Ewe Mungu wangu! Nifunike kwa rehema Zako.

وَارْزُقْنِي فِيهِ التَّوْفِيقَ وَالْعِصْمَةَ

Niruzuku tawfiki na hifadhi.

وَطَهِّرْ قَلْبِي مِنْ غَيَاهِبِ التُّهْمَةِ

Na utakase moyo wangu dhidi ya giza la shaka.

يَا رَحِيماً بَعْبَادِهِ الْمُؤْمِنِينَ

Ewe Uliye Mrehemevu kwa waja Wake waumini.

MWEZI THELATHINI:

اللَّهُمَّ اجْعَلْ صِيَامِي فِيهِ بِالشُّكْرِ وَالْقَبُولِ

Ewe Mungu wangu! Ijalie Saumu yangu iwe ni yenye kukubaliwa na kuthaminiwa.

عَلَى مَا تَرْضَاهُ وَيَرْضَاهُ الرَّسُولُ ،

Yenye kulingana na yale uyaridhiayo na ayaridhiayo Mtume.

مُحْكَمَةً فُرُوعُهُ بِالْأَصُولِ

Na ambayo matawi yake yameshikana madhubuti na shina.

بِحَقِّ سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ وَآلِهِ الطَّاهِرِينَ

Kwa haki ya bwana wetu Muhammad na Aali zake watoharifu.

وَالْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

Na kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa viumbe.

DUA YA MIKESHA KUMI YA MWISHO

Vile mwezi wa Ramadhani unapoingia hatua yake ya mwisho, waumini wanatambua kwamba zile neema zilizotolewa ndani ya mwezi huu zinafikia mwisho.

Wanaomba kwamba mwezi huo usingekwisha bila ya wao kusamehewa na kujibiwa.

Dua hii ina namna ya haraka ndani yake, kana kwamba mwito wa mwisho usio na matumaini kabla ya mwezi huo unaponyoka zake.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.**

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ

**Ewe Allah! Mrehemu Muhammad na Aali
Muhammad.**

اللَّهُمَّ إِنَّكَ قُلْتَ فِي كِتَابِكَ الْمُنْزَلِ

**Ewe Mungu wangu! Hakika Wewe umesema ndani ya
Kitabu Chako ulichokiteremsha:**

شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ هُدًى لِّلنَّاسِ
وَبَيِّنَاتٍ مِّنَ الْهُدَى وَالْفُرْقَانِ

“Ni mwezi wa Ramadhani ambao humo iliteremshwa
Qur’an kuwa mwongozo kwa watu, na dalili zilizo
wazi za mwongozo na upambanuzi.”

فَعَظَّمْتَ حُرْمَةَ شَهْرِ رَمَضَانَ بِمَا أُنزِلَتْ فِيهِ مِنَ
الْقُرْآنِ

Ukaitukuza heshima ya mwezi wa Ramadhani kwa
sababu ya ile Qur’ani uliyoiteremsha humo,

وَخَصَّصْتَهُ بِلَيْلَةِ الْقَدْرِ

Ukaufanya makhsusi kwa usiku wa Laylatul-Qadri,

وَجَعَلْتَهَا خَيْرًا مِنْ أَلْفِ شَهْرٍ

Nao ukaufanya ni bora kuliko miezi elfu.

اللَّهُمَّ وَهَذِهِ أَيَّامُ شَهْرِ رَمَضَانَ قَدْ انْقَضَتْ

Ewe Mungu wangu! Hivi sasa siku za Mwezi wa
Ramadhani zimekwisha,

وَلِيَالِيهِ قَدْ تَصَرَّمْتُ

Na nyusiku zake zimetuacha,

وَقَدْ صِرْتُ يَا إِلَهِي مِنْهُ إِلَى مَا أَنْتَ أَعْلَمُ بِهِ مِنِّي

**Nawe ewe Mola wangu wajua zaidi kuliko mimi ni
hadhi gani niliyofikia humo.**

وَأَحْصَى لِعَدَدِهِ مِنَ الْخَلْقِ أَجْمَعِينَ

**Nawe ndiye uwezaye kuhesabu idadi yake kuliko
viumbe wote.**

فَأَسْأَلُكَ بِمَا سَأَلْتَ بِهِ مَلَائِكَتَكَ الْمُقَرَّبُونَ

**Nakuomba kupitia yale waliyokuomba malaika Wako
wakuruba,**

وَأَنْبِيَائُكَ الْمُرْسَلُونَ، وَعِبَادُكَ الصَّالِحُونَ

Manabii Wako wajumbe na waja Wako wema,

أَنْ تُصَلِّيَ عَلَيَّ مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ

Umrehemu Muhammad na Aali Muhammad.

وَأَنْ تَفُكَّ رَقَبَتِي مِنَ النَّارِ

Na uniepushe na moto,

وَتُدْخِلْنِي الْجَنَّةَ بِرَحْمَتِكَ

Na uniingize Peponi kwa rehema Zako.

وَأَنْ تَتَفَضَّلَ عَلَيَّ بِعَفْوِكَ وَكَرَمِكَ

Na unifanyie fadhila kwa msamaha Wako na ukarimu Wako.

تَتَقَبَّلَ تَقَرُّبِي وَتَسْتَجِيبَ دُعَائِي

Kubali kujikurubisha Kwangu na jibu dua yangu.

وَتَمَنَّ عَلَيَّ بِالْأَمْنِ يَوْمَ الْخَوْفِ

Nikirimu kwa kunipa amani siku yenye khofu,

مِنْ كُلِّ هَوْلٍ أَعَدَدْتَهُ لِيَوْمِ الْقِيَامَةِ

Dhidi ya kila lenye kutisha uliloliandaa kwa ajili ya siku ya Kiyama.

إِلَهِي وَأَعُوذُ بِوَجْهِكَ الْكَرِيمِ

**Ewe Mola wangu! Najilinda kupitia heshima Yako
tukufu,**

وَبِجَلَالِكَ الْعَظِيمِ

Na utukufu Wako wenye nguvu,

أَنْ يَنْقُضِيَ أَيَّامُ شَهْرِ رَمَضَانَ وَلِيَالِيهِ

**Zisiishe siku za mwezi wa Ramadhani na nyusiku
zake,**

وَلَكَ قِبَلِي تَبِعَةٌ أَوْ ذَنْبٌ تُوَاخِذُنِي بِهِ

**Bila kunisamehe haki au dhambi utakayoniadhibu
kwayo.**

أَوْ خَطِيئَةٌ تُرِيدُ أَنْ تَقْتَصِّهَا مِنِّي لَمْ تَغْفِرْهَا لِي

Au kosa utakalolipiza kwangu bado haujanisamehe.

سَيِّدِي سَيِّدِي سَيِّدِي

Bwana wangu, Bwana wangu, Bwana wangu,

أَسْأَلُكَ يَا لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ

**Nakuomba ewe Ambaye hapana Mungu wa haki ila
Wewe,**

إِذْ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ

Kwani hakuna Mola wa haki ila Wewe.

إِنْ كُنْتَ رَضِيتَ عَنِّي فِي هَذَا الشَّهْرِ فَازِدْ عَنِّي رِضًا

**Ikiwa umeniridhia ndani ya mwezi huu basi niongezee
ridhaa Yako.**

وَإِنْ لَمْ تَكُنْ رَضِيتَ عَنِّي فَمِنَ الْآنَ فَارْضَ عَنِّي

Na ikiwa hujaniridhia basi tokea sasa niridhie.

يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ

Ewe Mbora wa warehemevu.

يَا اللَّهُ يَا أَحَدُ يَا صَمَدُ

**Ewe Allah, ewe Mmoja wa pekee, ewe Mwenye
kukusudiwa.**

يَا مَنْ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ

Ewe Ambaye hakuzaa wala hakuzaliwa.

وَلَمْ يَكُنْ لَهُ كُفُوًا أَحَدٌ

Wala hana yeyote anayefanana naye.

KITHIRISHA MANENO HAYA:

يَا مُلَيِّنَ الْحَدِيدِ لِدَاوُدَ عَلَيْهِ السَّلَامُ

Ewe uliyelainisha chuma kwa ajili ya Daud, amani iwe juu yake.

يَا كَاشِفَ الضُّرِّ وَالْكَرْبِ الْعِظَامِ عَنْ أَيُّوبَ عَلَيْهِ
السَّلَامُ

Ewe uliyeondoa madhara na shida kubwa kwa Ayyub, amani iwe juu yake.

يَا مُفَرِّجَ هَمِّ يَعْقُوبَ عَلَيْهِ السَّلَامُ

Ewe uliyemfariji Yakub, amani iwe juu yake.

يَا مُنْفِسَ غَمِّ يُوسُفَ عَلَيْهِ السَّلَامُ

Ewe uliyemuondolea simanzi Yusuf, amani iwe juu yake.

صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ

Mrehemu Muhammad na Aali wa Muhammad,

كَمَا أَنْتَ أَهْلُهُ أَنْ تُصَلِّيَ عَلَيْهِمْ أَجْمَعِينَ

Kama unavyostahili kuwarehemu wote.

وَأَفْعَلْ بِي مَا أَنْتَ أَهْلُهُ وَلَا تَفْعَلْ بِي مَا أَنَا أَهْلُهُ

Nifanyie yale unayostahiki, wala usinifanyie yale ninayostahili.

DUA YA USIKU WA MWEZI ISHIRINI NA MOJA

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema,
Mwenye kurehemu.**

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ

**Ewe Mungu wangu! Mrehemu Muhammad na Aali
Muhammad.**

يَا مُوَلِّجَ اللَّيْلِ فِي النَّهَارِ

Ewe Mwenye kuutia usiku katika mchana

وَمُوَلِّجَ النَّهَارِ فِي اللَّيْلِ

Na Mwenye kuutia mchana katika usiku.

